

**MADA**

**UHAKIKI WA FANI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA: NADHARIA  
YA UMUUNDO //**

**NA;**


**MURAGE JOYCE N.**

**C50/78806/2009**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI,**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**TANSIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (MA) KATIKA KISWAHILI**



**SEPTEMBER, 2011**

**UNGAMO**

**TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJAWAHI KUTOLEWA  
KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE  
CHOCHOTE.**



**MURAGE JOYCE N.**

**(Mtahiniwa)**

10/11/2011

**TAREHE**

**WASIMAMIZI**



**DKT. KINEENE WA MUTISO**

11/11/11

**TAREHE**



**DKT. RAYYA TIMAMMY**

11<sup>th</sup> Nov 2011

**TAREHE**

## **TABARUKU**

Kazi hii ninaitabarukia watoto wangu Julie, Marura, Mwangura na Wakio, ambao wamenivumilia sana nikiwa masomoni. Mmекуwa marafiki wangu wa dhati. Aidha, ninamtabarukia mzazi wangu mpendwa Julia Murage kwa kujinyima ili kunielimisha na kunihimiza tangu nikiwa mchanga hadi sasa. Umekuwa mwalimu wangu mkuu.

## **SHUKURANI**

Imekuwa safari ndefu mno tangu nilipoanza masomo haya hadi sasa nimefika kikomo. Safari yenye we imekuwa na panda shuka nyingi sana. Kufanikiwa kwa kazi hii hakungewezekana kama si juhudhi na kujitolea kwa watu mbalimbali na pia usaidizi na ushauri wao umenifikisha hapa.

Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha na uhai hadi kufikia sasa. Kama si mapenzi yake, nisingekuwa hai. Asante sana Mwenyezi Mungu.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Kineene wa Mutiso na Dkt. Rayya Timammy. Ushauri wao, usaidizi, uelekezi, kujitolea kwao na pia kuvumilia kwao ndiko kumeniwezesha kufanya kazi nzuri sana.

Aidha ninawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Isimu na Lughaa, kwa maarifa mliyonilimbikizia. Wahadhiri hasa walionifunza ni pamoja na Prof. Wamitila, Prof. Habwe, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Iribi, Dkt. Mweri na Bw. Mungania. Ninashukuru pia Dkt. Mbuthia na Dkt. Oduor kwa kunipa ushauri wa hekima kuhusu kozi hii.

Ninawashukuru pia wasomi wenzangu tulioshirikiana na kushauriana nao kuhusu masuala mbalimbali ya kiusomi. Wao ni Joyce Karinge na Pamella Tambasi. Wengine tulioshirikiana darasani ni pamoja na Nyaga, Watuha, Muhanda, Mwiraria, Mukaria, Mbula, Kitali, Oluga, Apopo, Amos, Kinyua, Mwanjala, Ngunjiri, Njuguna, Too na Mburu. Asanteni.

Ninawashukuru kwa dhati ndugu zangu Joshua, Dianah Kangard na mama yangu kwa kujitolea kunifadhili katika masomo yangu. Kujitolea huku ndiko kumenifikisha katika kina hiki cha

elimu. Bila wao nisingeweza kufika kiwango hiki cha masomo. Ninawaombea nyote mema duniani na pia ahera.

Ninamshukuru mama yangu mpendwa, Bi. Murage. Ninakushukuru ewe mama kwa kunifunza thamani ya uadilifu na bidii kutoka utotoni mwangu, shulen i hadi kukomaa kwangu. Nitakushukuruje kwa kunipa msingi bora tena imara katika safari hii ya maisha? Bidii yako ya mchwa na ari ya kukabiliana na changamoto za maisha ndizo zilizonifinyanga nikawa nilivyo. Asante sana mama, Mungu akujalie mema.

Kwa wanangu, ninawashukuru kwa kunihimiza bila kuchoka na kunisadikisha kuwa nitafuzu. Julie, Mungu akujazie, akushehenezee baraka zake, kwani umekuwa zaidi ya mama kwa ndugu zako. Maneno hayatoshi kukushukuru. Mungu akujalie mema pia.

Kwa mume wangu Mzame Fadhili, ukiwa katika masafa ya mbali, baini kuwa ndoto yangu ya kusoma inaelekea kutimia. Mungu akubariki pia.

Ninawapa shukurani marafiki zangu wote ambao wamekuwa wakinihimiza hasa nilipokuwa naelekeea kufifia na kufa moyo. Hususan, Pamella Muhanji, amenisaidia sana kwani amekuwa akinishikilia nafasi yangu kazini bila kuchoka. Ana wema usiomithilika. Pam, Mungu akubariki siku zote kwa ukarimu wako. Umenifaa zaidi ya ndugu.

Ninawashukuru Hannah na Julie. Walijitolea kunipigia chapa kazi zangu zote za kiusomi. Aidha, ningependa kumshukuru Sharon (Campus Mall) kwa kusaidia kupiga chapa tasnifu hii. Shukrani pia ni kwa Patrick Okombo kwa kuisoma kazi hii mwishoni. Mungu awanyeshee baraka zake.

Kwenu nyote ambao sikuwataja kwa majina na mlinifaa kwa njia moja au nyingine, ninawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. Tena sana.

## MUHTASARI

Utafiti huu unahusu uhakiki wa fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Nakala tunayotumia ni ya H.E Lambert katika (Bulletin No.23 of the East African Inter-territorial Language Committee). Utendi huu unaaminiwa kuwa ilitungwa na Fumo Liyongo katika mwaka wa 1517. Tunatumia nadharia ya Umuundo.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Katika sura ya kwanza, tumejadili masuala ya utangulizi wa utafiti. Tumezungumzia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumejadili misingi ya uhakiki wa fani. Tumeeleza maana ya fani na kutoa vipengele vyake mbalimbali. Pia tumeeleza kuwa tunashughulikia vipengele vifuatavyo katika *Utendi wa Mwana Ninga*: Ploti, muundo, mandhari, wahusika, usimulizi, toni na matumizi ya lugha.

Katika sura ya tatu, tumehakiki ploti na muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumbaini kuwa msuko au ploti ya utendi huu ni sahili. Msuko huu ni wa moja kwa moja na unaeleweka kwa urahisi. Pia tumeona kuwa muundo wa utendi huu unafuata kaida za utunzi wa tenzi.

Katika sura ya nne, tumehakiki mandhari na wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeona kuwa mandhari ni ya Uswahilini na pia Uarabuni. Pia ni mandhari ya baharini na msituni. Vilevile, tumeona kuwa wahusika ni wawili: Fumo Liyongo na Mwana Ninga.

Katika sura ya tano, tumehakiki matumizi ya lugha, toni na usimulizi katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeangalia smatumizi ya uhuru wa mshairi na tamathali za usemi. Tumeona kuwa

tamathali za usemi zinazotumiwa zinaingiliana na mandhari na vilevile sifa za urembo ambazo mtunzi anazisimuli. Kutokana na matumizi ya lugha, tumeona kuwa toni ya utendi huu ni ya mapenzi, furaha matumaini na imani. Usimulizi umetawaliwa na nafsi ya tatu, umoja. Tumeona kuwa mtunzi amefaulu katika matumizi ya fani na kutunga utendi wenye mshikamano.

Katika sura ya sita na ya mwisho, tunatoa hitimisho na mapendekezo mbalimbali ya utafiti zaidi. Kutokana na utafiti huu tumbaini kuwa vipengele mbalimbali vya fani vinavyotumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga* vimeingiliana na kuhusiana katika ujenzi wa umbo na muundo wa utendi wenyewe na vilevile kuwasilisha maana. Mintarafu ya hayo, tunahitimisha kuwa mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu katika utunzi wake.

Tunapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu kipengele cha usimulizi katika utendi huu. Pia uhakiki zaidi kuhusu fani katika utendi huu unaweza kufanya kwa kutumia nadharia tofauti.

## **YALIYOMO**

## **UKURASA**

Mada.....	i
Ungamo.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukurani.....	iv
Muhtasari.....	vi
Orodha ya yaliyomo.....	viii

## **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Tatizo la Utafiti.....	1
1.2 Madhumuni ya utafiti.....	2
1.3 Sababu za kuchagua mada hii .....	2
1.4 Upeo na mipaka.....	3
1.5 Nadharia tete .....	3
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili .....	3
1.7 Misingi ya nadharia .....	5
1.8 Njia za utafiti .....	7
1.9 Hitimisho .....	7

## **SURA YA PILI:**

### **MISINGI YA UHAKIKI WA FANI**

2.0 Utangulizi .....	8
2.1.0 Dhana ya Fani.....	8
2.1.1 Msuko / ploti .....	8
2.1.1.1 Aina za msuko .....	11
2.1.2.0 Muundo .....	12
2.1.2.1 Muundo wa ndani .....	13
2.1.2.2 Muundo wa nje .....	13

2.1.2.2.1	Beti .....	14
2.1.2.2.2	Mishororo .....	14
2.1.2.2.3	Mizani .....	14
2.1.2.2.4	Vina .....	15
2.1.2.2.5	Vipande .....	15
2.1.2.2.6	Kibwagizo .....	16
2.1.2.2.7	Bahari .....	16
2.1.3	Mandhari .....	17
2.1.4	Wahusika .....	19
2.1.5.0	Matumizi ya lugha .....	20
2.1.5.1.0	Uhuru wa kishairi .....	22
2.1.5.1.1	Ukiushi wa kimofolojia .....	22
2.1.5.1.2	Ukiushi wa kisintaksia .....	23
2.1.5.1.3	Ukiushi wa kimsamiati .....	24
2.1.5.2.0	Tamathali za usemi .....	24
2.1.5.2.1	Sitiari .....	25
2.1.5.2.2	Tashibihi .....	26
2.1.5.2.3	Chuku .....	26
2.1.5.2.4	Tasifida .....	26
2.1.5.2.5	Usambamba .....	27
2.1.5.2.6	Tashihisi .....	27
2.1.5.2.7	Takriri .....	28
2.1.5.2.8	Nidaa .....	29
2.1.6.	Toni .....	29
2.1.7	Usimulizi .....	30
2.2.	Hitimisho.....	32

## **SURA YA TATU:**

### **MSUKO NA MUUNDO KATIKA *UTENDI WA MWANA NINGA***

3.0	Utangulizi .....	33
3.1	Msuko katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	33

3.2 Muundo katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	37
3.3 Hitimisho .....	41

## **SURA YA NNE:**

### **MANDHARI NA WAHUSIKA KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

4.0 Utangulizi .....	42
4.1 Mandhari katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	42
4.2 Wahusika katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	44
4.2.1 Fumo Liyongo .....	45
4.2.2 Mwana Ninga .....	47
4.3 Hitimisho .....	50

## **SURA YA TANO:**

### **MATUMIZI YA LUGHA, TONI NA USIMULIZI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

5.0 Utangulizi .....	51
5.1.0 Matumizi ya lugha katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	51
5.1.1.0 Uhuru wa kishairi .....	51
5.1.1.1 Inkisari .....	52
5.1.1.2 Mazida .....	54
5.1.1.3 Tabdila .....	54
5.1.1.4.0 Uhuru wa kimsamiati .....	55
5.1.1.4.1 Msamiati wa Kiarabu .....	56
5.1.1.4.2 Msamiati wa Kingozi .....	57
5.1.1.4.3 Msamiati wa Kiamu .....	57
5.1.1.4.4 Uhuru wa kisintaksia .....	59
5.1.2.0 Tamathali za usemi .....	60
5.1.2.1 Sitiari .....	61
5.1.2.2 Tashibibi .....	63
5.1.2.3 Chuku .....	65

5.1.2.4	Usambamba .....	68
5.1.2.5	Tashihisi .....	69
5.1.2.6	Nidaa .....	69
5.1.2.7	Tasifida .....	70
5.1.2.8.0	Takriri .....	71
5.1.2.8.1	Takriri irabu .....	72
5.1.2.8.2	Takriri konsonanti .....	72
5.1.2.8.3	Takriri Silabi .....	73
5.1.2.8.4	Takriri Neno .....	74
5.2	Toni katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	75
5.3	Usimulizi katika <i>Utendi wa Mwana Ninga</i> .....	77
5.4	Hitimisho .....	80

## **SURA YA SITA:**

### **TATHMINI NA MAPENDEKEZO**

6.0	Utangulizi .....	82
6.1	Kuhusu madhumuni ya utafiti .....	82
6.2	Kuhusu nadharia tete .....	84
6.3	Mapendekezo ya utafiti .....	85
<b>Marejeleo</b>	.....	<b>86</b>
<b>Muswada wa</b>	<b><i>Utendi wa Mwana Ninga</i></b> .....	<b>92</b>

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.0 UTANGULIZI**

Utafiti huu unahu su uhakiki wa fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika sura hii ya kwanza, tunajadili masuala ya kiutangulizi ya utafiti huu. Masuala tunayoyazingatia ni madhumuni ya tasnifu, upeo na mipaka na nadharia tete. Vilevile, tunayachambua yaliyoandikwa kuhusu mada hii, misingi ya kinadharia na njia za utafiti. Masuala haya ni muhimu sana kwani yatatupa mwongozo thabiti katika utafiti wetu.

#### **1.1 TATIZO LA UTAFITI**

Tatizo la utafiti huu ni kuhakiki matumizi ya fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Fani huhusisha vipengele muhimu ambavyo huipa kazi ya kisanaa muundo maalum. Vipengele vya fani pia vina uamili mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa katika kazi ya kisanaa. Mbali na hayo, matumizi mazuri ya vipengele mbalimbali vya fani huipa kazi ya kifasihi mvuto wa uzuri wake. Kwa upande mwingine, matumizi mabaya ya fani huifanya kazi ya kifasihi kupoteza usanii na uzuri wake.

Msanii anapoamua kuteua vipengele fulani vya kisanaa lazima viweze kuvutia hadhira, kuzitekenya na kuathiri hisia zao. Hivyo, fani inakuwa ni kigezo cha kufana au kutofana kwa mtunzi katika usanii wake. Mtunzi wa ushairi huhitaji ufundi wa hali ya juu ili kuweza kufikia kilele cha ubunifu wa wake.

## **1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU**

Madhumuni ya utafiti huu ni kuhakiki fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika harakati za uhakiki huu, tunadhamiria kutekeleza yafuatayo:

- i) Kubainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali nya fani ambavyo vinatumika katika *Utendi wa Mwana Ninga*.
- ii) Kutathmini mchango wa vipengele nya fani katika kuwasilisha maana katika *Utendi wa Mwana Ninga*.
- iii) Kutathmini kufana au kufeli kwa msanii katika muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga*.

## **1.3 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI**

Tumechagua somo hili kwa sababu mbalimbali. Kwanza kabisa, *Utendi wa Mwana Ninga* ni mionganoni mwa tendi za kale mno kutungwa katika ushairi wa Kiswahili. Kulingana na Wamitila (2008), utendi huu wenyе beti 51 unasemekana kutungwa na Fumo Liyongo mnamo mwaka wa 1517. Kutoчana na ujadi wake, utendi huu unaainishikau mionganoni mwa tendi za zamani zilizowekea msingi ushairi wa Kiswahili. Japo utendi huu ni muhimu sana katika historia ya ushairi wa Kiswahili, hakuna utafiti wa kina na kiutalaamu uliofanywa. Waandishi mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili kama vile Knappert (1979) na Harrow (1991) wameugusia tu utendi huu bila ya kuufanya uchunguzi wowote wa kina.

Sababu ya pili ya kuchagua utendi huu ni kuwa ulitungwa na Fumo Loyongo. Fumo Liyongo ni mtunzi wa kutajika katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Jina la Fumo Liyongo limetajika katika tungo za kinathari hasa ngano za kale. Pia Fumo Liyongo ametunga mashairi kadha ya

Kiswahili. Kutokana na hayo, tumeteua kuhakiki utendi huu ili kutathimini kufana kwa mtunzi huyu katika utunzi wake.

#### **1.4 UPEO NA MIPAKA**

Tasnifu hii inahu uuhakiki wa fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Kwa kuwa dhana ya fani ni pana na ina vipengele vingi, tumechagua kuhakiki baadhi yavyo ambavyo ni ploti/msuko, muundo, wahusika, mandhari, toni, usimulizi na matumizi ya lugha.

Tunajadili namna vipengele hivi vyta fani viliviyotumiwa, uamili wake kiumbuji, mwingiliano na mahusiano yake, na mchango wake katika uwasilishaji maana na katika muundo au umbo la kazi nzima. Tunajikita katika *Utendi wa Mwana Ninga* na tunatumia muswada wa Lambert. Hatutashughulikia maudhui ila tu pale tutalazimika katika kufafanulia fani.

#### **1.5 NADHARIA TETE**

Nadharia tete za utafiti huu ni kama ifuatavyo:

- i. Vipengele vyta fani katika *Utendi wa Mwana Ninga* vimeingiliana na kuhusiana katika ujenzi wa utendi wenyewe.
- ii. Vipengele vyta kifani viliviyotumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga* vimechangia pakubwa katika uwasilishaji wa maana katika utendi huu.
- iii. Mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu katika usanifu wa fani hususan muundo katika utendi huu.

## **1.6 YALIOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI**

Mengi yameandikwa kuhusu dhana ya fani katika fasihi ya Kiswahili. Yaliyoandikwa kuhusu dhana hii yanapatikana sio tu katika vitabu bali pia katika tasnifu mbalimbali. Katika sehemu hii, hatutajadili haya. Tutazungumzia dhana ya fani katika sura ya pili.

Hali kadhalika, tafiti kadha zimefanywa kuhusu tenzi za Kiswahili. Tafiti hizi zilianza kitambo. Waliofanya utafiti katika tenzi za kale ni pamoja na Jan Knappert (1967, 1971, 1979), Lambert (1965), Hichens (1972), Lyndon Harries (1962), Allen (1971), mionganî mwa wengine. Wengi wa wasomi wa fasihi ya Kiswahili wamepuuza mchango wa watafiti hawa katika fasihi ya Kiswahili. Euphrase Kezilahabi (1997:59) anaeleza kuwa,

“....wale wataalamu wa kizungu ambao wamejitahidi sana na kukiendeleza na kukikuza Kiswahili walikuwa na ujuzi mdogo sana wa fasihi. Wao walikuwa wataalamu wa lugha na hawakuweza kufanya lolote zaidi ya kukusanya maandishi kadha ya Kiswahili na kuyatfsiri katika lugha zao kwa manufaa yao wenyewe. Kwa upande wa lugha, walifanya mambo mengi mazuri”.

Hata hivyo, ni maoni yetu kuwa watafiti hao wazungu walichangia katika kuwekea msingi utafiti katika tenzi za Kiswahili.

Pamoja na utafiti wa watafiti wa kizungu, kuna uhakiki uliofanywa majuzi kuhusu tenzi za kale na wasomi kama vile Mulokozi (1999), Kineene wa Mutiso (1985, 1996), Tom Olali (2004) na wengineo.

Mbali na hayo, hakuna utafiti wa kina kuhusu *Utendi wa Mwana Ninga*. *Utendi wa Mwana Ninga* umetajwa tu hapa na pale na wahakiki na waandishi mbalimbali. Wamitila (2008:226) anadokeza tu kuwa baadhi ya wataalamu wanassema kwamba *Utenzi wa Mwana Munga*

unaodaiwa kutungwa na Fumo Liyongo katika mwaka wa 1517 unaaminiwa kuwa utungo wa kwanza wa kishairi kutungwa. Maelezo ya Wamitila yanatusaidia kujua mwaka na mtunzi wa utendi huu. Hata hivyo, sisi tunashughulikia uhakiki wa utendi huu.

Mulokozi, (1999: vii) anamnukuu Ridhiwani (1996: 22-32) akieleza kuwa utungo wa Fumo Liyongo wa kale uliotiwa katika maandishi unaitwa “*Swifa ya Mwana Manga*” au “*Kumsifu Yang'a*”. Nukuu hili linatusaidia kujua mtunzi wa utendi huu. Hata hivyo, Mulokozi anaeleza mengi kuhusu Liyongo bila kuhakiki *Utendi wa Mwana Ninga*.

Knappert, (1979:84) ametafsiri *Utendi wa Mwana Ninga* kwa Kingereza na kuutolea maelezo mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha. Maelezo ya Knappert hasa yanahusu mtazamo wa jamii na dini ya Kiislamu kuhusu masuala mbalimbali katika utendi huu. Hakuna nadharia yoyote ambayo imetumiwa katika maelezo ya Knappert. Hata hivyo, maelezo haya yanatufaa katika kueleza baadhi ya sitiari zinazotumika. Katika utafiti wetu, tunahakiki utendi huu kwa undani na kuonyesha matumizi ya fani.

Kofa Tola (2009:46) anadai kuwa mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* hakufuata arudhi ya vina na mizani. Kwa maoni yetu, hoja hii si kweli kwani kila ubeti una mishororo minne (a,a,a,x. b,b,b,x. c,c,c,x.) n.k. Ambapo, a,b, na c hubadilika lakini x haibadiliki. Kila kina cha mishororo mitatu ya kwanza kinafanana ingawa kinabadilika katika kila ubeti. Lakini kina cha mshororo wa mwisho kutoka ubeti wa kwanza hadi wa 51 hakibadiliki. Kwa hivyo maoni yetu ni kuwa utendi huu unafuata arudhi ya vina na mizani na bahari ya ‘-nga’ kama kanuni za tenzi za kawaida.

Mohammad Kijumwa aliuainisha utungo huu kama utumbuizi. Naye Lambert akauita *Ode to Mwana Munga*. Nakala hii ndiyo tutakayo ichanganua na kuishughulikia (Nakala ya Bulletin

No.23 of East African Inter-Territorial Language Committee.) Tulichagua utungo huu kwa sababu ndiyo uliotuvutia zaidi kati ya tenzi zingine tulizofundishwa na kuzijadili darasani.

### **1.7 MSINGI WA KINADHARIA**

Nadharia tunayoitumia ni Umuundo. Nadharia ya Umuundo iliibuka nchini Czechoslovakia mwishoni mwa miaka ya ishirini. Nadharia ya Umuundo iliasisiwa na wasomi kama vile Roman Jakobson, N.S Trubetzkoy, Jan Mukarovsky, Boris Tomaserky. Roman Jakobson alikuwa amehama Ujerumani baada ya kupigwa marufuku kwa Urasimu. Wasomi hawa walibuni kundi lililojulikana kama Shule ya Isimu ya Prague na wakaitumia kuendeleza mawazo yao.

Kama anavyoeleza Culler, (1975: 4-5), waasisi wa Umuundo walitumia mawazo ya mwanaisimu Ferdinand de Saussure ambaye alibuni dhana mbalimbali za kiisimu na akawafundisha wanafunzi wake kupitia kwa miadhara mbalimbali. Mawazo ya de Saussure yalichapishwa na wanafunzi wake wakiongozwa na Charles Bally katika “*A Course in General Linguistic*” (1916).

Dhana zilizobuniwa na Saussure ni pamoja na ‘Langage’ (Lugha ijulikanayo na kutumiwa na jamii), ‘Langue’ (sheria na kanuni za lugha) na ‘Parole’ (matumizi ya lugha katika mazungumzo na maandishi). Wanaumuundo walitumia dhana hizi kusitiza kuwa, ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, mhakiki anafaa kuchunguza matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipengele vyake na mahusiano yake. Wanaumuundo walieleza kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama ‘langue’ na una kaida zake. Hivyo, kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni bia za utanzu zinazoitawala. Kwa mfano, katika kuhakiki *Utenzi wa Tambuka*, sharti tuchanganue lugha ilivyotumiwa vilevile sheria au kaida zinazotawala utenzi wa utenzi na kuona ikiwa mtunzi alitekeleza hizo sheria.

Waasisi wa Umuundo walitumia dhana za Saussure za kiashiria na kiashiriwa na wakaeleza kuwa lugha huundwa kwa viashiria na viashiriwa. Wanaumuundo wanaviona vipengele vya fani kama viashiria. Maana inayotokana na vipengele hivi vya kimtindo ndivyo viashiriwa.

Waanzilishi wa Umuundo walihakiki mashairi na tungo zingine za kifasihi. Walichunguza upatanifu wa sauti, vina, mizani, kiimbo, wizani na arudhi kwa jumla. Katika tungo za kimasimulizi, walisistiza umbo la msuko, hadithi na umbuji wa wahusika. Pia waliangalia mbinu za kifani kama vile jazanda, taswira, tashihisi, sadfa na ukiushi. Walieleza kuwa matumizi ya hali ya juu ya mbinu hizi huitofautisha lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida na taaluma nyingine.

Wanaumuundo walieleza kuwa kufaulu kwa kazi ya kifasihi hutokana na mbinu za kifani ambazo mtunzi anazitumia. Waliamini kuwa uhakiki wa kazi ya kifasihi haufai kuwa na urejelezi wa nje. Waasisi wa Umuundo walijali zaidi muundo wa kazi ya kifasihi kuliko mandhari ya kijamii ya kazi hiyo. Pia walipuuza kuhusisha fasih na mtunzi wake.

Tunaona kuwa mawazo ya nadharia hii yatatuufaa kuhakiki vipengele mbalimbali vya kifani vya *Utendi wa Mwana Ninga*.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu umekuwa wa maktabani. Tulisoma mashairi na tenzi mbalimbali za kale. Tulichagua *Utendi wa Mwana Ninga* ambao ni wa kale na haujatafitiwa. Pia tuliangalia jinsi una usanii wa hali ya juu. Pia tulisoma kuhusu nadharia ya Umuundo na kubainisha sifa zake kutoka maktabani. Tulidurusu pia tahakiki zingine kuhusu tenzi na fani. Tulitumia yaliyomo katika mtandao kuhusu nadharia yetu ya Umuundo. Hatimaye tulianza uchambuzi wa *Utendi wa Mwana Ninga*.

## **1.9 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumejadili juu ya tatizo la utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu za kuchagua somo, pia tumeshughulikia upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu somo na msingi wa nadharia ambayo ni Umuundo na mwishowe tukajadili njia tulizozitumia katika utafiti wetu ambapo tulijikita sana matabani na katika mtandao.

## **SURA YA PILI**

### **MISINGI YA UHAKIKI WA FANI**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya kwanza, tiliyajadili masuala yanayohusiana na utangulizi wa utafiti wetu. Katika sura hii, tunajadili misingi ya kinadharia ya fani. Tunajadili dhana ya fani, kubainisha vipengele vyake mbalimbali na kuonyesha uainishaji wake. Tunatoa mifano ya kijumla kutoka katika ushairi wa Kiswahili. Dhana ya fani ni pana na inajumulisha vipengele vingi mno. Tunajadili tu vipengele ambavyo tutavitumia katika uhakiki wa *Utendi wa Mwana Ninga* katika sura zijazo.

#### **2.1.0 DHANA YA FANI**

Wataalamu na wahakiki wa fasihi wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Wataalamu hawa ni pamoja na Mbatiah (2001), Wamitila (2003) na wa Mutiso (2005).

Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu. Maudhui na fani. Maudhui ni masuala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Maudhui pia hujulikana kama yaliomo. Kwa upande mwingine, fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui.

Mbali na kuyawasilisha maudhui, fani pia huwa na uamilifu wa kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi. Umbo lenyewe linaweza kuwa la ndani au nje. Katika tungo za kishairi, umbo la ndani hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, wahuksika, mandhari, msuko,

usimulizi, toni na kadhalika. Kwa upande mwingine, umbo la nje hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile beti, mishororo, mizani, vina na kadhalika.

Utafiti wetu unahusu uchanganuzi wa masuala haya yote. Wataalamu wa nadharia ya Umuundo wanastitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani. Katika kufasiria matini na kupimia kufana au kufeli kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii.

Vipengele vya fani ni vingi. Vile tunakavyovishugulikia katika utafiti huu ni pamoja na msuko/ploti, wahusika, usimulizi, toni, muundo, mandhari na matumizi ya lugha.

### **2.1.1 MSUKO/PLOTI**

Msuko ni mojawapo wa vipengele muhimu vya kifani katika kazi za kifasihi. Wamitila (2003) anasema kuwa msuko ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kurejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na huhusisha matendo ya nguli na jinsi yanavyowaathiri wahusika wengine. Msuko huelezea namna matukio haya yanavyofuatana kiusababishi. Wamitila anaendelea kuelezea kuwa istilahi hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Aristotle alipoongea kuhusu muundo wa tanzia. Baadhi ya sifa za kimsingi zinazohusiana na msuko unaojenga kazi ya fasihi ni pamoja na ukubalifu, taharuki, mgogoro, matumaini au matarajio, usababishi na tokeo, mantiki, mshutukizo na mvuto.

Kwa upande mwingine, Ngara (1985) anasema kuwa uti wa mgongo wa kazi ya kifasihi ni msuko. Maoni haya yana maana kuwa msuko hushikilia vipengele vingine vya kazi ya kifasihi na kuvipa muundo. Kwa hivyo, msuko ni msururu wa matukio yaliyopangwa kiwakati. Matukio haya huwa na uhusiano wa kiusababishi na kutegemeana katika suluhu.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, tunapata mambo muhimu yanayofafanua msuko kama ifuatavyo:

- i. Mpangilio: Ni lazima msanii atue na kuyapanga matukio yake kulingana na azma ya msuko wa kazi yake.
- ii. Mfululizo wa vitendo: Vitendo vyenyewe vinaanzia mwanzoni mwa kazi inayohusika na kuendelea kwa uhusiano wa kimantiki hadi kufikia mwisho wa kazi yenye. Tukio moja haliwezi kuunda msuko mzima. Kwa hivyo, lazima matukio mbalimbali yawepo ndio yajenge msuko ikiwa hadithi inayosimuliwa ni ya kimatendo. Lazima kuwepo mwanzo wa matukio, kati na mwisho katika mwingiliano wa nguvu zinazokinzana na aghalabu hii humaanisha kuwepo visa vitatu au zaidi. Matukio haya hukua moja baada ya jingine. Tukio la pili likifuata kwa uhusiano wa kiusababishi kutoka kwa tukio la kwanza, na la tatu likifuata kwa uhusiano huo kutoka kwa la pili. Katika hadithi yenyе msuko wa matukio uliofungamana, tukio moja likiondolewa tu, basi hadithi nzima itakuwa imeumbuliwa. Ni muhimu kutambua pia matukio ya mwanzo yanaweza kupelekwa mwisho na ya mwisho kuletwa mwanzo na pia kuwa na msuko mkuu na mingine midogo midogo. Msuko wa aina hii huwa changamani.
- iii. Uhusiano wa vitendo ni tokeo la mwingiliano wa nguvu na nguvu nyingine. Yamkini, pasipo mgogoro au ukinzani msuko au ploti haitakuwepo. Nazo nguvu za nafsi na za nje lazima ziweze kuonyesha ukinzani. Ukinzani huu ndio unaofungamanisha tukio moja kwa tukio lingine. Ndio unaimarisha uhusiano wa kiusababishi unaojenga mapambano.

Mapambano ya nguvu kwa nguvu, wakati mwingine hufikia kilele katika tukio moja, na baada ya hapo kunaweza kuwa na taharuki.

Msuko, ukiwa mpangilio wa matukio hulenga kwenye maisha, huku ukichagua wahusika wachache, migogoro michache na visa vichache kutoka kwa kapu kubwa lenye sampuli nyingi. Uchaguzi huo huwa wa vitu vyenye mshikamano wa pamoja na unaolenga mwisho mmoja. Msuko ni elementi inayotambulishwa sana na riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Vilevile, unaweza kujitokeza vizuri katika ushairi na hasa utendi kwa sababu ya kipengele cha hadithi.

#### **2.1.1.1 AINA ZA MISUKO**

Kimsingi kuna aina mbili kuu za msuko. Msuko sahili na msuko changamano. Msuko sahili ni aina ya msuko ambao ni wa moja kwa moja. Hoja hii ina maana kuwa msuko sahili huwa unatiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Matukio hufuatana kiwakati na kiusababishi. Msuko sahili hauna urejelezi wa nyuma. Aghalabu, msuko wa aina hii hupatikana katika tungo fupi kama vile hadithi fupi na vilevile mashairi. Tendi fupi za Kiswahili pia huwa na msuko wa aina hii. Kulingana na Wamitila (2003) msuko sahili pia hujulikana kama msuko msago.

Kwa upande mwingine, msuko changamano ni aina ya msuko ambao huenda mbele na nyuma. Hoja hii ina maana kuwa msuko wa aina hii hutumia mbinu rejeshi kwa wingi. Kutokana na hali hii, msuko changamano huwa na taharuki kwa kiwango cha juu sana. Taharuki hii huwapa wasomaji hamu ya kuendelea kusoma zaidi na zaidi ili wapate kufuatilia hadithi husika na kupata maana.

Kulingana na Wamitila (2003), msuko changamano huweza kujumuisha aina nyinginezo za msuko kama vile msuko mkuu, msuko kinzani, msuko linganuzi, msuko msago, msuko rudufu na msuko kaida.

Msuko mkuu hutumiwa kurejelea matukio yanayotendwa na kumzunguka mhusika mkuu katika kazi ya kifashi. Msuko wa aina hii huwa ndicho kiini cha kazi ya kifasihi. Kwa upande mwengine, msuko kinzani hutumiwa kurejelea matendo yanayotendwa na kumzunguka mhusika mkuu mpinzani. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Ayub*, msuko kinzani unahu su matukio na matendo yanayomzunguka ibilisi ambaye ni mpinzani wa Ayub.

Kimsingi msuko changamano huwa na urejelezi mwangi. Kulingana na Ngara (1985), msuko huu pia hujulikana kama msuko wa kioo. Msuko wa aina hii huwa na kipengele cha wakati na vipengele kama vile wahusika na usimulizi ambapo lazima kuwepo na mahusiano ya vipengele hivi na matukio ambayo yanatendwa katika nyakati tofautitofauti. Nyakati hizi zinapowasilishwa katika hadithi lazima ziwe katika wakati uliopita, uliopo na hata ujao; na huu muundo ndio unaoleta urejeshi katika hadithi.

## **2.1.2.0 MUUNDO**

Mbatiah (2001:59) anaeleza kuwa muundo ni uhusiano wa elementi za kazi ya kifasihi katika mpangilio thabiti unaozishikamanisha elementi hizo. Maeleo ya Mbatiah yanaoana na yale ya Wamitila (2003) ambaye anasema kuwa dhana hii (ya muundo) hutumiwa kueleza sifa za nje zinazoipa kazi ya kifasihi sura za kutambulikana. Hata hivyo, si lazima elementi za kumuundo ziweze kuonekana kijuujuu. Baadhi ya elementi hizi huwa za kindani. Kutokana na sababu hii, sharti hadhira isome kazi inayohusika ili kubaini na kuelewa elementi hizo. Hali hii husababisha

kuwepo kwa aina mbili kuu za miundo katika kazi za kifasihi. Muundo wa ndani na muundo wa nje.

### **2.1.2.1 MUUNDO WA NDANI**

Muundo wa ndani ni aina ya muundo wa kazi ya kifasihi ambao hauonekani kwa macho. Hujumuisha vipengele ambavyo sharti hadhira isome kazi ya kifasihi ili iweze kuvibaini. Kimsingi, muundo wa ndani hujengwa kutokana na mwingiliano baina ya vipengele mbalimbali vya kifani kama vile wakati, toni, usimulizi, wahusika na kadhalika. Kwa hivyo, muundo wa ndani ni dhana inayoingiliana sana na dhana ya msuko, yaani mfuatano wa matukio na mahusiano yake kiwakati na kiusababishi.

### **2.1.2.2.0 MUUNDO WA NJE**

Muundo wa nje ni aina ya muundo wa kazi ya kifasihi ambao huonekana na kutambulika kwa kutazama. Muundo wa nje ndio hurejelewa kama umbo la kifasihi. Hadhira inaweza kutambua vijenzi vya muundo wa nje wa shairi kwa kilitazama tu. Si lazima walisome shairi hilo. Hoja hii inaelezewa vizuri na Mohammed (1995) anaposema kuwa umbo linajengwa na vipengele vinavyoungana pamoja kujenga kitu kimoja kikuu. Mohammed anaendelea kueleza kuwa katika shairi, vipengele hivyo ni beti, vipande, mishororo, mizani, vina na kibwagizo.

### **2.1.2.2.1 BETI**

Beti ni migao mbalimbali ya shairi. Migao hii inaweza kulinganishwa na aya za tungo za kinathari. Beti za mashairi ya arudhi huwa ni migao ya idadi maalum ya mishororo. Shairi linaweza kuwa na idadi yoyote ya beti ilmuradi tu litekeleze azma yake. Kuna baadhi ya

mashairi ambayo yana beti chache sana. Hata hivyo, tenzi ni aina ya mashairi ambayo huwa na idadi ya juu ya beti. Kwa mfano, *Utenzi wa Rasil'Ghuli* una beti 4,584. Kwa upande mwingine, *Utendi wa Mwana Ninga* una idadi ya chini ya beti nazo ni 51.

#### **2.1.2.2.2 MISHORORO**

Mishororo ni mistari mbalimbali ambayo hupatikana katika kila ubeti wa shairi. Aina tofauti za mashairi huwa na idadi tofauti za mishororo katika ubeti. Kulingana na kaida au arudhi za mashairi ya kimapokeo, kila shairi sharti liwe na idadi maalum ya mishororo. Hivyo, idadi ya mishororo inakuwa kigezo cha kuainisha mashairi katika aina zake. Kwa mfano, shairi lenye beti mbili huitwa tathnia /mathnawi / uwili. Vilevile, mashairi yenye mishororo minne katika kila ubeti hujulikana kama tarbia.

#### **2.1.2.2.3 MIZANI**

Mizani ni mapigo ya kisauti au silabi zinazopatikana katika mshororo wa kila ubeti. Mizani inaweza kuwa irabu moja tu au ikawa ni silabi yenye muungano wa konsonanti moja au zaidi na irabu moja. Idadi ya mizani katika kila mshororo huweza kutofautiana kutoka aina moja ya shairi hadi aina nydingine. Kutokana na kigezo hiki cha idadi ya mizani katika mshororo wa kila ubeti, tunaweza kupata aina tofauti za mashairi kama vile kisarambe (mizani kumi na moja), tendi (mizani 6, 8, 11); gungu (mizani kumi) na kadhalika. Haya ni kulingana na Wamitila (2008) na Abedi (1954).

#### **2.1.2.2.4 VINA**

Vina ni mfanano wa mizani unaotokea katika sehemu ya katikati au mwisho wa kila mshororo. Kulingana na Wamitila (2008: 257) urudiaji unaotokea katika sehemu ya mwanzoni mwa mishororo unaweza kujumlishwa hapa kwa kuwa kimsingi unaonyesha mfanano wa mizani. Hata hivyo, tunalionna pendekezo hili la Wamitila kuwa geni na hivyo linalofaa kufanyiwa utafiti zaidi. Sisi tunachukulia vina kuwa aina ya urudiaji wa sauti unaotokea mwishoni mwa mishororo katika tenzi. Beti mbili zifuatazo ni mifano ya vina katika *Utenzi wa Mwanakupona*:

Negema, wangu binti,

Mchachefu, wa sanati,

Upulike, wasiati,

Asaa kuzingatiya.

Maradhi yamen shika,

Hatta yametimu mwaka,

Siyapata kutamka,

Neno lema kukwambiya.

(ubeti 1-2)

#### **2.1.2.2.5 VIPANDE**

Vipande ni migao inayopatikana katika mishororo ya tungo za kishairi. Kunayo mashairi yenye mgao mmoja, miwili na hata mitatu. Mashairi huru hayana vipande vya mishororo vyenye ubainifu kama mashairi jadi. Kwa upande mwingine, mashairi ya kimapokeo yana sifa ya kugawika kwa mishororo kama mojawapo ya kaida zake. Kwa mifano, aina ya mashairi ya

ukawafī huwa na vipande vitatu katika kila mshororo. Beti za tenzi huwa na kipande kimoja pekee.

#### **2.1.2.2.6 KIBWAGIZO**

Kibwagizo ni istilahi ya kishairi ambayo hutumiwa kurejelea mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa shairi fulani ambao umerudiwa kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kibwagizo huwa ni muhimu sana katika kufasiri dhamira ya shairi husika. Hivi ni kusema kuwa kibwagizo hubeba ujumbe maalum wa shairi hilo na husisitiza ujumbe huo. Hata hivyo, si mashairi yote yaliyo na kibwagizo. Mashairi yasiyo na kibwagizo huwa na kiishio. Mashairi ya aina hii huwa na dhamira yake kutokana na maudhui. Kibwagizo huweza kuchukuliwa na kufanywa kichwa cha shairi.

#### **2.1.2.2.7 BAHARI**

Bahari ni kina cha mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa utenzi. Kina hicho hurudiwa kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho wa utenzi. Utensi mmoja unaweza kuwa na bahari tofauti na utenzi mwingine. Kwa mfano, *Utenzi wa Rasi'lGħuli* una bahari ‘ri’ ilħali *Utenzi wa Fatumah* una bahari ‘a’. Uwezo wa kutosheleza kanuni ya bahari huwa ni mojawapo wa vigezo vyakupimia umahiri wa mtunzi wa utenzi fulani.

Tunapoangazia suala la umbo la shairi, tunapata kuwa kuna mashairi yale yaliyotungwa na wanamapokeo yaliyofuata arudhi mahususi. Mashairi haya hutungwa kwa kuzingatia mpangilio maalum wa beti, idadi fulani ya mizani, upatanishi wa vina, vipande, mishororo na kibwagizo. Baadhi ya watalamu wanaouna mkono utunzi huu ni Shabaan Robert (1968), Amri K. Abedi (1954), Mathias Munyampala (1965) na wengineo.

Katika miaka ya 1960, kulizuka mgogoro katika maumbo ya mashairi. Watunzi kama vile Mazrui na Shariff (1976), Kezilahabi (1974), Mulokozi (1975) na wengineo walikuwa baadhi ya Wanamapinduzi na pia waasisi wa mashairi huru. Mashairi haya huru huwa na maumbo maalum pia kwa sababu watunzi huzingatia mipangilio ya sentensi, kama unyumbuaji wa maneno. Pia kuna jinsi vifungu vya mistari hupangwa ili kuibua hisia nzito ya kishairi. Kwa hivyo, kila kazi ya kishairi ni lazima iwe na umbo lake lililoundwa na msanii wa kazi husika.

### 2.1.3 MANDHARI

Wamitila (2003) anasema kuwa dhana hii hutumiwa kurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia, yaani mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Katika mapana, dhana hii hutumiwa kuelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa fasihi. Aghalabu, wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia.

Mandhari katika ushairi huibuka na kuenda pamoja na matukio pasi na maelezo ya kina ya mandhari. Mandhari yafaa yahusishwe pamoja na mila na itikadi za jamii, dini na utamaduni na sio kuhusishwa na mazingira tu, katika tendi.

Mandhari yaweza kuhusisha mahali mbalimbali kama vile duniani, ahera, porini, msituni, pangoni, mlimani, peponi na kadhalika. Mazingira nayo humwezesha msomaji kuelewa taswira ya msanii. Mazingira yaweza kuwa ya kivita, kisiasa, kidini, kimpenzi, kijamii, kimapinduzi, kiuchumi na kadhalika.

Mandhari huweza kuwa ya ukinzani au usambamba na msanii hutumia haya kuwasilisha ujumbe wake. Kwa mfano, anaweza kuwasilisha maisha ya umasikini na pia ya utajiri na taswira hizi

mbili (hali duni na hali ya kifahari) tukazipata kwa njia wazi sana. Kipengele cha mandhari ni muhimu kwani huwa na jukumu la kisitiari, kiuelezi, kihisishi, kitaashira na kidhibiti halihamasa. Kulingana na Wamitila (2002), mandhari huwa kama kipengele cha kiutanzu, kidhibiti cha wahusika na mandhari kama majaliwa. Yaani, maeleo ya msanii kuhusu mahali fulani katika kazi yake yanaweza kutuonyesha mwelekeo maalum wa hadithi.

Gill (1985) asema kuwa mandhari ni neno pana linalojumlisha mahali ambapo wahusika wamewasilishwa, muktadha wa kijamii, wahusika, kama vile familia, marafiki, matabaka, tamaduni, imani na kaida za jamii kitabia. Mandhari huchangia katika kueleza mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali waliiyomo na hata husaidia katika kutambua maudhui yaliyo katika kazi ya kifasihi.

Gill (1985) na Wamitila (2002) wameongea juu ya upana wa mandhari. Wamesema kwamba mandhari si mazingira tu bali hurejelea masuala mengi yakiwemo itikadi, mila, desturi, jamii na vilevile elimu. Hivi ni kusema mandhari huweza kuhamishwa katika mazingira tofauti kulingana na muktadha. Tukiangazia tenzi, *Miraji na Fatuma* (mbinguni), *Herekali*, *Siri li Asirali* (kivita). Kwa hivyo ni wazi kuwa mandhari huwa mapana.

Elementi zinazotengeneza mandhari ni kama hali ya kijiografia (kimazingira) pamoja na hali ya kihistoria (kiwakati) au kipindi maalum (msimu wa mwaka). Mandhari pia hujengwa kwa mazingira ya kijumla ya mhusika yaani hali yao ya kidini, kiakili na kijamii.

Tumeangazia maoni ya wataalamu tuliovataja hapo juu kuhusu dhana ya mandhari na hapo tukapata kuwa mandhari ni mahali na wakati ambapo matukio ya hadithi hufanyika.

Mandhari husaidia katika kuhakiki wahusika. Mandhari pia huibua hisia fulani na kutupa taswira kamili ya hali iliyopo.

## 2.1.4 WAHUSIKA

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Katika fasihi, matendo ya viumbe hawa hufanana na yale ya binadamu. Wataalamu kama Mbatiah (2001), wa Mutiso (2005) na Wamitila (2003) wanadai kuwa wahusika ni watu, vitu, wanyama, ndege, wadudu, miti, mashetani, majini na kadhalika wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe. Kutokana na matendo na mazungumzo yao, wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.

Kulingana na maelezo ya wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa kila mhusika akiwa ameshikilia jukumu lolote lile, ana umuhimu mkubwa sana katika kazi ya sanaa. Yeye hupenyezwa katika nafasi yake maalum ili kutimiza malengo maalum ya msanii hata kama amepewa nafasi finyu sana, hataonekana kana kwamba kazuka kiajali.

Wahusika wengine hushirikishwa kwa kupewa nafasi ya kutenda, kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira. Kusawiriwa kwa mhusika kutategemea na msanii na nia yake ya kumfanya kuwa kielelezo cha wema au ubaya katika jamii. Mhusika husawiriwa kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kihalisia.

Kama tulivyoona hapo juu, wahusika ni vivuli wanaochukua nafasi za wahusika halisi. Msanii anapowasawiri wanyama, wadudu, ndege na vitu visivyo na uhai vitende kama binadamu halisi huwa na malengo mbalimbali. Kwanza, hutumia mafumbo au huwfumba wasomaji anapotaka kujikinga kutokana na mazingara kama vile ya kisiasa yasiyofaa. Athari za wahusika huonekana kutokana na matendo ya wahusika vivuli.

Kulingana na Forster (1927), wahusika wako katika makundi mawili makuu, wahusika bapa na duara. Wahusika bapa huwa hawabadiiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Kuna aina mbili za

wahusika bapa, bapa sugu na bapa vielezo. Bapa sugu ni wale ambao wanajulikana kutokana na maelezo ya masanii. Jinsi wanavyoelezwa na mwandishi ni ile ile katika utokeaji wao wote. Wahusika bapa - vielezo hawabadiliki pia, na hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo yao na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielezo cha kifupisho cha wasifu wao. Wahusika duara hukaribiana na binadamu wa kawaida, mabadiliko yanayowajia ndio husababisha uduara kwa mifano ya kisaikolojia, kijamii na kiukuaji. Mhusika duara anamwakilisha binadamu halisi lakini wakati mwingine huzua sifa zisizolingana na binadamu wa kawaida. Tukiangazia tenzi kama za mitume na mashujaa wengine, tutapata sifa hizi za kiajabu katika matendo yao.

Aristotle (1965), alisema kuwa lazima mhusika aonyeshe hali ya juu ya kimaadili. Zamani, fasihi ilitazamwa katika misingi ya kimaadili ambayo ilipaswa kuwa ya hali ya juu, tena, lazima mhusika apewe sifa zinazohusiana na kushikamana vizuri na matendo yake, lazima sifa zake zimtambulisse kama mhusika, awe kama binadamu na awe na uthabiti ulio bayana.

### **2.1.5.0 MATUMIZI YA LUGHA**

Wanaisimu wanakubaliana kwamba lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenyе utamaduni unaofanana kuwasiliana (Wamitila 2003). Hoja hii ina maana kuwa dhima kuu ya lugha ni mawasiliano. Lugha yaweza kuwa ya mazungumzo, maandishi au ishara. Wanajamii huwa na njia yao ya kawaida ya matumizi ya lugha. Wataalamu wa fasihi kama vile Syambo na Mazrui (1992) wameirejelea lugha itumiwayo katika maingiliano ya kila siku ya wanajamii kuwasiliana kama lugha ya kawaida.

Tofauti na shughuli za kila siku za jamii fasihi ina lugha yake ambayo hutofautiana kwa kiasi fulani na lugha ya kawaida. Lugha ni kipengele muhimu sana cha kifani katika ushairi kwani hutofautisha utanzu huu na tanzu nyingine.

Sifa za matumizi ya lugha hutokana na sifa za ushairi wenyewe. Waasisi wa nadharia ya Umuundo walisisitiza haja ya upekee wa lugha ya kishairi. Walieleza kuwa kilichopo si washairi bali ni ushairi. Kama njia ya kusisitiza umuhimu wa matumizi ya lugha ya kishairi, Kitula na Amata (2001: 5) wanaeleza kuwa;

...shairi ni chombo mwafaka kinachomwezesha mwandishi kuufumbata upana wa maisha katika maneno teule machache yaliyofinyangwa kisanaa. Uteuzi huo wa maneno hupangiliwa kama vito kwenye kazi ya Sonara anayefua chombo cha dhahabu. Vito kwenye jicho la mvaaji na mtazamaji. Mpangilio wa maneno teule katika ushairi hujenga picha na tashbihi inayojenga maana na mantiki inayochorwa na mshairi, lakini heba yake imo katika kukamilisha hisi kwa msomaji au msikilizaji, kama hisi za mapenzi, chuki, dhiki, faraja, ari au mapuuza, ujinga au werevu, sifa au tashtiti pamoja na kumzindua.

Hata hivyo, Kitula na mwenzake wanaendelea kueleza kuwa;

...ingawa ushairi ni pambo la lugha na usanifu, mashairi hayawezi kuwa yenye mvuto iwapo hayahu hisia na mambo yanayowafahamikia wote waishiyo katika jamii inayohusika.

Kulingana na Wamitila (2008:228) mchanganuzi wa mashairi anapaswa kuijuliza maswali kadha. Je, msamiati anaoutumia mshairi ni msamiati wa kawaida au msamiati maalum? Je, ikiwa msamiati ni mwepesi au mzito ni athari gani inayochwa na msamiati (na uteuzi wake) huo? Je,

msamiati huo unaathiri vipi maana ya kifasihi katika shairi lenyewe? Je, msamiati huo una umbo la kawaida? Je, yapo maneno maalum ambayo yanaathiri uelewekaji wa shairi linalohusika? Je, maneno yanayotumiwa yana uwezo wa kuibua maana nyingine ya ziada katika shairi? Pamoja na masuala haya yanayohusiana na msamiati, mhakiki vilevile anafaa kuchunguza matumizi ya uhuru wa kishairi na tamathali za usemi.

#### **2.1.5.1.0 UHURU WA KISHAIRI**

Mbatiah (2004:95) anaeleza kuwa dhana ya uhuru wa kishairi ina maana mbili zinazohusiana. Kwanza, ni uhuru wa mshairi kukiuka kaida na kanuni za matumizi ya lugha katika viwango vya kimofolojia, kisintaksia, kimsamiati na kisemantiki. Pili, ni uhuru wa mwandishi wa utanzu wo wote kukiuka sio tu kaida na kanuni za lugha bali pia kaida za kijamii na kweli za kihistoria. Maeleo ya Mbatiah ni muhimu sana kwani yanaonyesha kuwa dhana ya uhuru wa kishairi ni pana zaidi kuliko namna inavyojulikana na kutumiwa na wahakiki wengi wa fasihi ya Kiswahili. Watu wengi wamechukulia tu kuwa uhuru wa kishairi unaishia tu katika ukiushi wa matumizi ya lugha ya kawaida. Hata hivyo, kwa sababu ya wakati tutaitumia dhana ya uhuru wa kishairi kwa mujibu wa kijelezi cha kwanza anachokitoa Mbatiah, kwamba, uhuru wa kishairi ni ukiushi wa matumizi ya lugha katika viwango vya mofolojia, sintaksia, msamiati na semantiki.

#### **2.1.5.1.1 UKIUSHI WA KIMOFOLOJIA**

Uhuru wa kimofolojia hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi katika uendelezaji wa maneno. Kuna takribani aina tatu za uhuru wa kimofolojia: inkisari, mazida na tabdila.

Inkisari ni aina ya ukiushi ambapo maneno fulani katika ushairi yanafupishwa ili kupata ulingano au kutosheleza idadi ya mizani inayohitajika na vilevile kupata urari wa vina. Inkisari pia huhusisha uunganishi wa baadhi ya maneno na kuyafanya yatamkwe kana kwamba ni neno moja.

Kwa upande mwingine, mazida huwa ni kinyume cha mbinu ya inkisari. Katika mazida, msanii hurefusha neno kwa kuongeza silabi ili kupata idadi ya mizani inayohitajika.

Hatimaye tabdila huhusisha kubadilisha kwa mwendelezo wa maneno na kuyafanya yatamkwe tofauti na yalivyozoleka. Tofauti na inkisari na mazida, tabdila haihusishi kuongeza au kupunguza idadi ya mizani katika neno. Kinachobadilika ni mwendelezo na vilevile matamshi. Dhima kuu ya tabdila ni kuongeza mvuto katika ushairi.

#### **2.1.5.1.2 UKIUSHI WA KISINTAKSIA**

Ukiushi wa kisintaksia ni aina ya uhuru wa kishairi ambapo mtunzi hukiuka miundo ya sentensi iliyozoleka ya lugha husika. Katika fasihi ya Kiswahili, mbinu hii hujulikana kama kuboronga sarufi au ‘mpinduo wa kisintaksia’. Mbinu hii pia huchukuliwa kuwa aina ya tabdila kutokana na sababu kuwa huhusisha kubadilisha sarufi ya lugha husika. Umahiri wa mtunzi katika kucheza na maneno na vilevile uwezo wake wa kuibusha miundo mbalimbali ya lugha huwa ni kitambulishi cha ukomavu wake katika matumizi ya lugha hiyo. Ukiushi wa kisintaksia pia ni kitambulishi cha sajili ya ushairi.

### **2.1.5.1.3 UKIUSHI WA KIMSAMIATI**

Ukiushi wa kimsamiati unahusisha matumizi ya msamiati tofauti na ule uliozoleka katika matumizi ya lugha ya kila siku. Washairi huwa na uhuru mbalimbali wa kimsamiati ukiwemo matumizi ya maneno ya lahaja tofauti na vilevile maneno ya Kiarabu. Ukiushi wa kimsamiati huashiria hali ya kubobe kwa mtunzi katika matumizi ya misamiati mbalimbali. Vilevile, misamiati hutambulisha mazingira yaliyoizaa kazi ya kifasihi. Pia hudokeza kuhusu asili ya mtunzi, mtazamo wake, tajiriba yake na kadhalika.

### **2.1.5.2.0 TAMATHALI ZA USEMI (UKIUSHI WA KISEMANTIKI)**

Tamathali za usemi ni mojawapo wa dhana kongwe zaidi katika fasihi za ulimwenguni. Dhana hii imetumika katika uhakiki wa fasihi tangu enzi za nadharia ya balagha ya zamani. Pamoja na hayo, dhana hii imeelezwa na kuainishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi katika makamusi na pia vitabu vya kinadharia.

Japo wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wameishughulikia dhana hii, uainishaji wake ambao ni wazi zaidi umefanywa na Kuhenga (1977) na Wamitila (2008).

Wataalamu hawa wanakubaliana kuwa tamathali za usemi ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa kimakusudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au iliyozoleka. Holman na Harmon (1986:203) wanaeleza kuwa ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au wa kimuundo.

Tamathali za usemi huwa ni mbinu ya kupimia usemi wa mtunzi. Ubunifu lazima ujitekeze katika matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi. Pia, tamathali za usemi huvutia wasomaji na

kuwapa hamu ya kutaka kusoma zaidi. Huwafanya wasomaji kutafakari kuhusu wanayoyasoma na kulinganisha na mazingira na mandhari yao.

Tamathali za usemi ni nyingi mno. Zile zinazochukua nafasi muhimu katika kazi za kifasihi na hasa ushairi ni pamoja na sitiari, tashibihi, kinaya, chuku, taashira, tashihisi, takrir, usambamba na nyinginezo. Kwa kuwa tamathali hizi ni nyingi, hatutaweza kuzijadili zote. Tutajadili tu zile ambazo zitatuzaa katika utafiti huu.

#### **2.1.5.2.1 SITIARI**

Sitiari ni tamathali muhimu sana ya usemi mionganini mwa tamathali za usemi. Tamathali hii hujitokeza sana katika kazi za kifasihi. Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili vyenye hulka tofauti bila ya kutumia vilinganisho. Katika sitiari, ulinganishaji huwa wa moja kwa moja. Kitu kimoja hutajwa kuwa kitu kingine. Kwa mfano, tukisema ‘Zawadi ni twiga’, tutakuwa tunamwita Zawadi twiga kama njia ya kulinganisha hali fulani ya Zawadi na twiga. Hali hiyo ni kama vile urefu.

Wamitila (2008:420) anaeleza kuwa sitiari huwa na muundo wenye sehemu tatu. Sehemu zenyewe ni kilinganishi, kilinganishwa na msingi wa ulinganishi. Kwa upande mmoja kilinganishi ni kitu ambacho hutumiwa kulinganishwa na kingine. Kilinganishwa ni kitu kinacholinganishwa na kitu kingine. Msingi wa ulinganishi ni sifa inayolinganishwa. Hivyo, katika mfano tuliofa wa ‘Zawadi ni twiga’, Zawadi ndicho kilinganishwa, twiga ni kilinganishi ilhali msingi ni sifa ya urefu wa twiga ambayo Zawadi analinganishwa nayo.

#### **2.1.5.2.2 TASHIBIHI**

Tashibihi ni aina nyingine muhimu ya tamathali za usemi. Tamathali hii hutumiwa kulinganisha vitu viwili vyenye hulka tofauti kama ilivyo katika sitiari. Hata hivyo, tofauti na sitiari, tashibihi hutumia viungo vya ulinganishaji kama vile ‘ja’, ‘mithili ya’, ‘mfano wa’, ‘sawa na’, ‘kama’, na kadhalika. Mifano ya tashibihi ni kama vile:

- i. Yohana ni mweusi kama makaa.
- ii. Tito ni mlafi kama fisi.
- iii. Kitambaa hiki ni cheupe ja pamba.

Sawa na sitiari, tashibihi ni tamathali ya usemi ya mlinganisho wa hulka.

#### **2.1.5.2.3 CHUKU**

Chuku ni mojawapo ya tamathali za usemi. Chuku pia hujulikana kama udamisi. Hutumiwa kurejelea hali ya kitu kuelezwu kwa namna inayoongeza au kupunguza sifa zake kimakusudi. Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitu kinachohusika hukiukwa. Kitu hicho huweza kudunishwa au kukuzwa. Katika Kiswahili chuku hujulikana kwa msemo ‘tia chumvi’.

#### **2.1.5.2.4 TASIFIDA**

Wamitila (2008:396) anaeleza tasifida kama mbinu inayotumiwa katika kazi za kifasihi kuficha ubaya, uozo au uovu fulani kwa kutumia maneno au lugha inayopunguza makali ya uozo, ubaya au uovu unaozungumziwa. Pamoja na hayo, tunaongeza kuwa tasifida huficha aibu au fedheha.

Lugha ya tasifida inaweza pia kupatikana kutokana na kutumia mbinu nyingine za lugha kama vile misemo na sitiari.

#### **2.1.5.2.5 USAMBAMBA**

Usambamba ni aina maalum ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali za usambamba. Miongoni mwa aina hizi ni usambamba wa kimuundo na usambamba wa kisintaksia.

Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika ushairi wa Kiswahili ambapo muundo sawa wa baadhi ya mishororo hurudiwa katika beti mbalimbali.

Kwa upande mwingine, usambamba wa kisintaksia ni aina ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao unahuusu urudiaji wa vipengele au vipashio vya kisintaksia katika mfuatano. Vipengele virudiwavyo, viwe virai au vishazi, hupatikana katika sehemu ile ile ya sentensi vikiwa vimeandamana.

#### **2.1.5.2.6 TASHIHISI**

Tashihisi ni aina nyingine muhimu ya tamathali za usemi ambapo vitu visivyokuwa na uhai hupewa sifa ya uhai. Tamathali hii pia hujulikana kama uhuishaji. Mara nyingi sifa hizo za uhai huwa zinalenga kuvitukuza au hata kuvitweza vitu hivyo. Matumizi hulenga kuukejeli uwezo wa binadamu juu ya vitu hivyo. Katika fasihi ya Kiswahili, vitu kama vile milima, jua, mvua, majabali na vinginevyo hupewa sifa za uhai. Wamitila (2008: 427) anaeleza kuwa tashihisi

inaweza kutazamwa kama aina ya sitiari kwa sababu ya kulinganisha vitu vilivyo hai na visivyo hai. Hata hivyo, sitiari ni ya moja kwa moja kinyume na tashihisi ingawa zote zinahusika na uhamishaji wa maana.

#### **2.1.5.2.7 TAKRIRI**

Takriri ni mojawapo wa tamathali za usemi ambayo inahusu urudiaji katika lugha. Ingawa urudiaji ni wa aina nyingi sana, baadhi za urudiaji umepewa majina mengine kama vile usambamba. Katika utafiti huu tutatumia dhana ya takriri kama urudiaji unaohusu sauti za lugha. Katika hali hii, tunapata urudiaji wa aina tatu kuu: takriri irabu, takriri konsonanti na takriri vina.

Takriri irabu inahusu urudiaji wa sauti ya irabu ileile katika neno au maneno ya mshororo mmoja yanayopakana. Urudiaji huu hupatikana katika tungo za kishairi na hudhamiriwa kuleta ridhimu katika shairi.

Takriri konsonanti vilevile hupatikana katika neno au maneno yanayopatikana katika mshororo. Vilevile, hupatikana katika mianzo ya maneno ya mishororo ya beti zinazopakana. Urudiaji huu vilevile huwa njia ya kudumisha ridhimu na kuonyesha umahiri wa mtunzi katika usanifu wake.

Kwa upande mwingine, takriri vina inahusu urudiaji wa vina vilevile katika mishororo ya ubeti au shairi lote. Takriri vina ni mojawapo wa kaida muhimu za mashairi ya kimapokeo. Urudiaji vina husaidia kuleta wizani katika mashairi.

#### **2.1.5.2.8 NIDAA**

Nidaa ni aina ya tamathali ya usemi inayohusu matumizi ya siyahi au maneno ya hisia. Maneno hayo yana uwezo wa kuibua hisia mbalimbali kama vile uchungu, hofu, woga, wivu, tamaa, na kadhalika. Mara nyingi nidaa huonyeshwa kwa kutumia alama hisi (!) baada ya neno. Pamoja na kuibua hisia katika kazi za kifasihi, nidaa huwa na uamilifu wa kuteka makini ya hadhira na kuonyesha mtazamo wa mtunzi.

#### **2.1.6.0 TONI**

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), toni ni dhana inayotumiwa kueleza mkabala alionao msimulizi wa hadithi kuhusu wahusika waliomo katika hadithi yake na yaliyomo, pia matukio na hali iliyopo. Aghalabu, toni au lahani huhusiana na masafa ujumi katika fasihi. Mawazo ya Wamitila ni ya kweli kwa sababu toni ni lazima ijitokeze katika kazi zote za kifasihi. Katika toni twapata lengo la msanii, tunapata kufasiri chuki kutoka kwa toni, huzuni, huruma, masikitiko, furaha, ukatili, kilio na uadilifu au uozo wa jamii.

Holman (1960) anasema kuwa toni pia yaweza kutumiwa kuonyesha hali ya kazi yenye ya sanaa pamoja na mbinu mbalimbali zinazotumiwa kuunda hali hiyo. Anaongeza kuwa katika hali kama hii, toni ni zao la mseto na hata kubadilika kwa vitu kama vina, takriri, ishara na vinginevyo.

Hivi ni kusema, toni yaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ikiwa imebadilika iwe ni katika kutilia mkazo jambo fulani katika takriri au katika ishara, toni italeta hisia mwafaka kulingana na uteuzi na upangaji wa maneno kimakusudi kutegemea hadhira na uhusiano wa msanii. Naye Richards (1964) anatalia mkazo kwamba toni ya matamshi yake msanii huakisi

ufahamu wa uhusiano huo na hisia zake juu ya anaowazungumzia. Richards anaendelea kusema kuwa toni ni mtizamo fulani alionao msemaji kuhusu msikilizaji. Nasi twaona kuwa msanii awe mwangalifu anapotumia maneno kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira yake ili yaibue hisia za kuridhisha.

Toni huwa mtazamo wa msanii anaochukuwa kuhusu wasomaji wake na masuala anayowasilisha. Naye msomaji huwa ni kama kioo cha wahakiki kwani wao hulinganisha hali ya msomaji na ile ya msanii. Leech na Short (1981) wanadai kuwa masafa ndiyo kiini cha ulinganishi huu wa toni (masafa rasmi, mazungumzo ya kawaida na uhusiano wa karibu). Wanasema kuwa msanii huteua masafa ya mbali kuonyesha uhusiano wa mbali au ya karibu, kuonyesha uhusiano wa karibu. Kama wanavyodai wataalamu hawa, kadri masafa yanavyokuwa mafupi, ndivyo toni hujitokeza wazi. Msanii ndiye huchagua masafa na hapo kudhibiti mwitikio wa msomaji, anapobadilisha mtindo wa toni yake katika kazi yake ya fasihi. Kwa kutamatisha tunasema kuwa, msanii hutumia toni kwa lengo la kuathiri hadhira, pia husaidia kupima au kuja hisia zinazosababishwa na kazi ya kifasihi inayohusika. Pia ni muhimu kusema kuwa nguvu ya toni itatambulikana kulingana na muktadha wa mazingira inapojitokeza. Osiemo (1997) anatilia mkazo kuwa lazima toni ikubaliane na wakati, mandhari na mwendelezo wa ploti.

#### **2.1.7.0 USIMULIZI**

Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Wamitila (2003) ameeleza aina mbalimbali za usimulizi nazo ni pamoja na, usimulizi anuwai, usimulizi ngazi, usimulizi maizi, usimulizi penyezi/dukizi, usimulizi sawia, usimulizi tangulizi, usimulizi wa kiitimamu, usimulizi wa ki-

utendi, usimulizi wa kirejeshi, usimulizi wa kiutomaji, usimulizi nafsi ya kwanza, usimulizi nafsi ya pili na usimulizi nafsi ya tatu.

Mawazo ya Wamitila ni kuwa kazi zote za fasihi lazima ziwe na matukio na hayo matukio yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia nyingi za usimulizi. Msimulizi hana budi kuchagua mtindo fulani amba ni wa kufaa zaidi kuwasilisha mawazo yake yatakayomwathiri msomaji kwa njia moja au nyingine. Usimulizi unaweza kuwa wa kufululiza matukio moja kwa moja bila ya kutatiza, au unaweza kuwa usimulizi wa kirejeshi na ule wa kiutomaji – ambapo msimulizi hukatiza mtiririko au hurejelea mambo yaliopita (kirejeshi) au aweza kukatiza mtiririko wa hadithi na kuweka vifungu kama vile barua. Hii aghalabu hutokea katika kazi ya kidrama (kiutomaji).

Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi anaweza kuwa mshiriki wa matukio au matendo ya hadithi au ashuhudie matendo hayo bila kushiriki. Msimulizi ambaye hashiriki na yuko nje ya hadithi anaweza kueleza hisia na fikra za wahusika wengine na matukio yote ya hadithini. Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza kuna mhusika ambaye anashiriki katika hadithi. Yeye huwa anajielezea tu tajiriba zake lakini hana uwezo wa kueleza za mtu mwengine. Msimulizi huyu huweza kujenga uhusiano wa karibu mno kati yake na msomaji. Sisi kama wasomaji tunaona anachoona, kusikia anachosikia na kuhisi anachohisi. Anaposimulia, yeye hutumia viwakilishi ‘mimi’ na ‘ni’ vya nafsi ya kwanza.

Usimulizi wa nafsi ya pili huhusisha viwakilishi vya nafsi ya pili ‘wewe’ na ‘u’. Kulingana na Wamitila (2003) ni kuwa aina hii ya usimulizi ni nadra sana kupatikana ingawa kuna mwandishi wa Marekani Kusini aitwaye Charles Fuentes aliandika riwaya iitwayo *The Death Of Artemio Cruz* na akatumia nafsi hii.

Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa na matumizi ya ‘a’ na ‘ye’ katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasanii. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani.

Welleck na Warren (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafsi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo kushiriki moja kwa moja; huwaacha wahusika pekee yao na kumruhusu msomaji kuwahakiki bila kumwelewa mwandishi. Usimulizi mwingine humruhusu msomaji kumwelewa mwandishi na mitazamo yake kuhusu mambo yanayoikabili jamii.

Welleck na mwenzake wanasema kuwa wahusika katika ushairi husemezana. Hii aghalabu huwa katika mashairi ya malumbano. Usimulizi wa matukio huweza kuwa wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Katika tendi, usimulizi ni muhimu sana kwani huwasilisha ufanuzi zaidi wa sifa za mandhari, wahusika wake, majukumu yao na matukio yakiwa katika mbinu ya mfululizo au kukatizwa kwa visa. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi msanii atakaowasilisha.

## 2.2 HITIMISHO

Katika sura hii, tumefafanua kwa kina baadhi ya vijenzi vya fani katika fasihi hususan tenzi ambavyo vinazitofautisha na kazi zingine za kifasihi. Ni matumaini yetu kwamba maoni ya wasomi na yetu pamoja yametoa msingi mwafaka katika uelewa wa utendi tunaoshughulikia.

## **SURA YA TATU**

### **MSUKO NA MUUNDO KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya pili, tulijadili misingi ya uhakiki wa fani. Katika sura hii, tunahakiki msuko na muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga*. Tutaanza kwa kujadili msuko na kisha muundo.

#### **3.1 MSUKO WA UTENDI WA MWANA NINGA**

Katika sura ya pili, tulieleza msuko ama ploti kama mfuatano wa matukio katika hadithi kiwakati na kiusababishi.

Msuko wa *Utendi wa Mwana Ninga* ni sahili au wa msago. Hadithi au masimulizi ya utendi huu yanatiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mtunzi hatumii mbinu rejeshi, hakuna uchangamano katika msuko huu.

Hadithi ya *Utendi wa Mwana Ninga* inahusu tukio la mtunzi, Fumo Liyongo kumsifu mpenzi wake, Mwana Ninga, Mwana Manga au Yanga.

Kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa sita, mtunzi anatoa dibaji. Anawaomba watu wapige pembe za nyati na tembo wachanga kuwaita watu wote (hata wanawake na watoto) wa mbali na wa karibu ili kwa pamoja waweze kumsifu Mwana Ninga. Jambo la kimsingi katika beti hizi sita za mwanzo ni kutoa kiini cha masimulizi.

Baada ya utangulizi huu, mtunzi anaanza moja kwa moja masimulizi yake. Tulivyoeleza masimulizi yake yanahu kumsifu mpenzi wake, Mwana Ninga. Anaanza kichwani ambapo

anaeleza kuwa nywele zake za singa ni hariri au laini. Pamoja na hayo, anaeleza kuwa kichwa chake ni kama marmar na utosi wake unameremeta. Akiwa bado kwenye kichwa, mtunzi anaeleza kuwa masikio ya Mwana Ninga ambayo ni shupavu katika kusikia yamepinda vizuri kama kombe la nanga. Mtunzi anaendelea kueleza kuwa uso wa Mwana Ninga umetengenea kwa uzuri, unapendeza na kuvutia, na kwamba hajawahi kuona mwingine unaotoa mwanga kama huo. Kuhusu nyusi za macho yake, msimulizi anaeleza kuwa zimelingana na kufungamana vizuri. Hakuna mwanya kati yazo wala hakuna ule ulio mrefu kuliko nyingine. Zote ziko mstari mmoja. Vilevile, nyusi zenyewe ni nyeusi mno, zaidi ya wino. Anazilinganisha na matanzu ya mti wa Munga.

Ni nyeusi mno,  
Zaidi ya wino,  
Zitwalie kono,  
Ya tandu za mnga.  
(ubeti. 12)

Pamoja na hayo, mtunzi anaeleza kuhusu macho ya Mwana Ninga. Anaeleza kuwa macho yake anapoyafumba na kisha kuyafumbua, humtisha mtu yejote anayemtazama. Pua yake inaelezwa kuwa ya ajabu na yenye mikunjo sita ya kupendeza. Mbali na pua, midomo yake inaelezwa kuwa myembamba na anaposema hata mjinga anamwelewa. Ndani ya kinywa chake meno yake yanametameta, hayana uchafu wowote wa kijani au wekundu. Meno haya yanalinganishwa na mwanga ambao unang'ara kutoka Manga. Ulimi wa Mwana Ninga unaelezwa kuwa mwepesi, na asemapo huwa anarudisha mwangwi angani.

Maelezo haya yanayohusu kichwa cha Mwana Ninga na sehemu zake mbalimbali yanatolewa katika beti za 7-22. Maelezo haya yanashheheni sifa ambazo mtunzi anaziona kuwa kitambulishi cha urembo wa mwanamke kichwani.

Baada ya maelezo ya kichwani, mtunzi anaendelea kueleza akiteremka shingoni. Anaeleza kuwa shingo ya Mwana Ninga ni ndefu kama mwanzo mkubwa, shingo yenye we imepambwa kwa aina mbalimbali za mapambo ikiwemo mikufu iliyotengenezwa vizuri. Mabega yaliyoshikamana na shingo ya Mwana Ninga vilevile yanaelezwa kuwa hedaya njema ambayo iliumbwaa na Mwenyezi Mungu na yamejaa nyama. Mabega yenye we yanaelezwa kuwa ya kadri au wastani, si makubwa wala madogo na yamelingana vyema. Maelezo haya yanayohusu shingo na mabega yanatolewa katika beti za 24-26.

Baada ya sifa za mabega, Fumo Liyongo anasimulia kuhusu mikono ya Mwana Ninga. Anaeleza kuwa mikono hiyo inaning'inia, viganja vimejaa nyama na vidole vyake ni virefu kama matanzu ya mti wa mnga. Kucha za vidole vyake vya mikono zinaleezwa kuwa na rangi ya kifani ambazo msimulizi anaapa kuwa hajawahi kuziona. Vilevile, makwapa yake yanaelezwa kuwa yaliyomea nywele kama mche wa mpakanga na hutoa harufu ya mafuta mazuri sawa na ya Uarabuni. Masimulizi haya yanayohusu mikono ya Mwana Ninga yanapatikana katika beti za 27-31.

Kuanzia ubeti wa 32-34, mtunzi anasimulia kuhusu uzuri wa kifua cha Mwana Ninga. Anaeleza kuwa kilichoumbwa kwa uzuri zaidi na tofauti na cha mwanamke mwingine ye yote. Msimulizi anaendelea kusimulia kuwa maziwa (matiti) ya Mwana Ninga yanapendeza sana kiasi cha kwamba hata yanapokuwa yamefunikwa nguo, yanashhtua macho. Kwa upande mwingine, yakifunuliwa nguo, akili zinatanga.

Napa siwenepo,  
Sishuhudiepo,  
Matunda ya Pepo,  
Yake Mwana Manga. (ubeti 32)

Yakiwa nguoni,  
Hutisha uyuni,  
Yawapo baiyani,  
Akili hutanga. (ubeti 33)

Beti za 32 na 33 zinadhihirisha namna mtunzi au msimulizi wa utendi huu anavyojivunia urembo wa mpenzi wake. Ni masimulizi yanayoelekeza kwa maudhui ya sifa.

Baada ya maelezo ya kifuani, msimulizi anaeleza kuhusu mbavu za Mwana Ninga ambazo ni nyororo sana na hushtua yejote mwenye kumsinga. Maungo ya mbavu hizi yamelala vizuri hayajitokezi, yamefunkwa vizuri na nyama ya mbavu zenyewe. Pamoja na hayo, tumbo lake lina mikunjo mizuri ya kupendeza na pia kitovu chake ni kama kikubwa kama sanduku dogo la sindano lenye asili ya ufundistadi wa Makka na yejote anayenuswa kitovu hiki, pua yake hupata uchepechepe wa damu na hung'ara huku ikivuja naye akiona kisunzi. (ubeti wa 34-37).

Katika ubeti wa 38-39, mtunzi anaeleza kuhusu kiuno kizito cha Mwana Ninga. Anasimulia kuwa kiuno hiki kimejitokeza, ni duara na kina wepesi wa kuzunguka kama dira. Msimulizi anaapa kuwa kamwe hajawahi kuona kiuno kingine kizuri sawa na hiki.

Katika ubeti wa 40-47, msimulizi anasimulia kwa njia ya kisitiari na kijazanda kuhusu sehemu za siri za Mwana Ninga na namna alivyofurahia aliposhiriki ngono naye. Anataja sehemu hiyo ya siri kama ‘safina’ ambayo alisafiria katika bahari ya mapenzi. Msimulizi anaeleza kuwa ‘safina’ yenyewe aliiona kwa macho (na kuikagua), si ndefu na si pana, ‘safina’ hiyo imejaa

nyonga na joto jingi sana, pia inanukia vizuri kama vumba la kutoka Makka. Sehemu hii ya utendi huu ndiyo kilele cha usimulizi. Hoja hii inatokana na sababu kuwa msimulizi anatumia lugha yenye uwezo wa kuibua hisia kali za tamaa ya mapenzi mionganini mwa hadhira.

Sehemu hii vilevile imetumia sitiari, jazanda na tashibiha za kibahari zinazotoa taswira ya tendo la kujamiiiana kati ya msimulizi na mpenzi wake. Pia inaweza kufasiriwa kumaanisha kuwa kwa mtazamo wa msimulizi, urembo wa mpenzi wake hauishii tu katika namna anavyoonekana bali pia namna anavyoshiriki mapenzi.

Katika beti za 48-51, mtunzi anahitimisha kwa kusimulia kuhusu sehemu za chini ya mapaja, kombe la magoti na vilevile nyayo zake. kwamba yote ni kazi ya nakshi.

Kufikia hapa, tunaona kuwa msuko wa *Utendi wa Mwana Ninga* ni sahili au wa msago. Mtunzi amesimulia moja kwa moja kuhusu anachokiona kuwa urembo wa mpenzi wake. Msuko huu umeendelezwa na kufungamana sana na kipengele cha usimulizi. Aidha, maudhui ya sifa na mapenzi yanafungamana na msuko huu. Ni kupitia kwa msuko huu pia ndipo tunapata sifa za wahusika wa utenzi huu na mtazamo wao. Pia, msuko huu unaendelezwa kupitia kwa mbinu ya taswira. Taswira inayotolewa ni ya mti wa Mnga na vilevile ya mifanyiko ya baharini.

### **3.2 MUUNDO WA UTENDI WA MWANA NINGA**

Katika sura ya pili, tulieleza kuwa kuna muundo wa ndani na wa nje. Muundo wa ndani katika ushairi unaingiliana na msuko. Katika sehemu hii, tunajadili muundo wa nje wa *Utendi wa Mwana Ninga*.

Muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga* umetosheleza kaida za utunzi wa utendi. Utendi huu una beti 51. Tofauti na baadhi ya tendi za jadi, utendi huu si mrefu sana. Mionganii mwa beti hizi, beti za kwanza sita ni za utangulizi. Usimulizi umeanzia ubeti wa 7 hadi ubeti wa 51. Kila ubeti wa *Utendi wa Mwana Ninga* umegawanywa katika mishororo minne yenye kipande kimoja. Kuwepo kwa kipande kimoja ni mojawapo ya sifa za tendi. Ufuatao ni ubeti wa saba kuonyesha mishororo.

Takwanda kitwani,

Nduza sikiani,

Hariri laini,

Zake nyele singa.

Kila mshororo wa *Utendi wa Mwana Ninga* una mizani sita, mifano tunautoa katika ubeti wa 14 ufuatao:

Pu-a-ye a-ja-bu,

1- 2-3 4-5-6

Zi- vu- ngu hu-re – bu,

1 – 2 – 3      4 – 5 – 6

Ni – si–ta hi- sa –bu

1 - 2 - 3 4 - 5 - 6

Mwe– nyi ku – zi– wa – nga

1 - 2      3 - 4 - 5 - 6

Mizani ni silabi zinazopatikana katika neno na huleta urari na mdundo fulani katika ushairi wa Kiswahili. Tenzi nyingi huwa na mizani minane katika kila mshororo. Hata hivyo, utendi wetu una mizani sita katika kila mshororo. Kuna tenzi zingine ambazo huwa na mizani 6, 8 na 11. Mfano wa mizani ni kama:

Ubeti 13      ma-to      a-vi-ka-po-      (mizani 6)

Kha-sa      a-vu-a-po      „      „

M-tu      a-ki-we-po      „      „

Hu-ti-sha      Ku- ye- nga      „      „

Msanii amezingatia kaida ya mizani sita katika utendi mzima. Jambo hili linaufanya utendi huu uweze kuimbika au kukaririka kwa yale mapigo. Aidha anatumia mbinu mbalimbali za uhuru wa kishairi ili kutosheleza mizani, kudumisha maana, mdundo na mahadhi ya utendi. Mbinu hizi ni kama inkisari, mazida n.k. Tutazichanganua na kuzitolea maana baadaye katika uhakiki wetu.

Vina vya *Utendi wa Mwana Ninga* vinafanana katika mwisho wa mishororo mitatu ya kwanza ya kila ubeti. Hata hivyo, vina vya ubeti mmoja ni tofauti na ubeti unaofuatia na havitiririki kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hali hii hutokea katika tenzi zote za Kiswahili. Mifano:

Ubeti 50;      Tafuze kadiri,

Hazi kudhihiri,

Kowa la zumari,

Taole kuzinga.

Ubeti 51; Nyaoze ashashi,

Vaole ni koshi,

Kazi ya nakishi,

Kwa kazi ya Manga

Katika beti 50 na 51 hapo juu mpangilio wa vina ni kama ifuatavyo:

50;

- a) ri,
- b) ri,
- c) ri,
- d) nga.

51;

- a) shi,
- b) shi,
- c) shi,
- d) nga.

Vina vya mishororo yote ya mwisho wa kila ubeti vimekaririka kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Kina chenyewe ni ‘nga’. Kina cha aina hii huitwa bahari. Hivyo, *Utendi wa Mwana Ninga* una bahari ‘nga’. Kama tulivyoeleza mwanzoni, kutosheleza idadi ya mizani ni mojawapo wa vigezo vya kupimia kufana kwa mtunzi katika usanii wake. Kutokana na hayo, tunaona kwamba mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu katika kutosheleza kaida muhimu za utunzi wa tendi.

Kwa kuwa tendi hazina kibwagizo ambacho tulieleza kuwa kinasaidia kufasiria dhamira katika ushairi, dhamira ya utendi huu inaweza kupatikana kutokana na kusoma utendi wenyewe kikamilifu. Mstari wa mwisho wa utendi huu ni kiishio au kimalizio

Kufikia hapa tunaona kuwa muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga* umesanifiwa kikaida na unaingiliana vizuri na matumizi ya lugha. Ingawa beti, mizani, vina, bahari na kimalizio ni vipengele vya kimuundo, vinaingiliana au kuhusu matumizi ya lugha na namna lugha hiyo inavyopangwa ili kupata muundo mahususi. Vilevile, muundo huo unaingiliana na msuko wa utendi huu kwani unahakikisha kuwa hadithi au masimulizi yanawekewa mipaka.

### **3.3 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumehakiki muundo na msuko wa *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeona kuwa msuko wa utendi huu ni sahili au wa msago. Msuko umetiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa njia sahili. Pia, tumeona kuwa muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga* umefuata kaida za utunzi wa tenzi. Mtunzi amefaulu kuoanisha muundo na msuko. Kutokana na msuko huo, tunapata maudhui ya sifa na mapenzi. Katika sura ifuatayo, tunahakiki vipengele vya mandhari na wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

## SURA YA NNE

### **MANDHARI NA WAHUSIKA KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

#### **4.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya tatu, tulihakiki msuko na muundo katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika sura hii, tutahakiki mandhari na wahusika katika utendi huu. Tutaanza na mandhari na hatimaye wahusika.

#### **4.1 MANDHARI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

Tulieleza mandhari kama muktadha wa mahali na kiwakati wa kazi ya kifasihi. Kazi za kifasihi huwa na vielekezi vinavyo elekeza kwenye muktadha huo wa kimahali na kiwakati. Vielekezi hivyo vinaweza kuwa vitu vya kimaumbile, wahusika, hali na hata matumizi ya lugha.

Kuhusu mandhari ya mahali, *Utendi wa Mwana Ninga* unaelekeza kwenye mseto wa mandhari ya Uswahilini na Uarabuni. Mandhari ya Uswahilini yanaonekana kutokana na matumizi ya lugha. Lugha inayotumiwa katika utendi huu ni mchanganyiko wa lahaja za Kiswahili. Kwanza, kuna maneno ya Kingozi ambayo ni lahaja ya zamani sana ya Kiswahili. Mifano ya maneno ya kingozi ni:

Ambo (katika ‘atakapokwamba’) – angalia (ubeti 17)

Wene (katika ‘siwenepo’) – ona (ubeti 32)

Vilevile kuna maneno ya lahaja nyingine kama vile Kiamu. Mifano ya maneno ya Kiamu ni kama yafuatayo:

Wanda – wanja (ubeti wa 20)

Kieuu – kidevu (ubeti wa 23)

Mato – macho (ubeti wa 13)

Miomo – midomo (ubeti wa 17)

Tandu – tanzu (ubeti wa 27)

Kitwani – kichwani (ubeti wa 7)

Maneno ya Kiamu ndiyo mengi. Hivyo, utendi huu umetungwa katika lahaja ya Kiamu izungumzwayo mjini Lamu. Mazingira halisi ya kutungiwa kwa *Utendi wa Mwana Ninga* ni Us wahilini katika maeneo ya visiwa vya Lamu.

Hali kadhalika, *Utendi wa Mwana Ninga* umesawiriwa katika mandhari ya baharini katika ubeti wa 40-47. Msimulizi anaeleza namna alivyofanya mapenzi/kushiriki ngono na mpenzi wake (Mwana Ninga) kwa kulinganisha na hali ya baharini. Hapa anatumia sajili ya baharini ili kuibua taswira yenye hisia na mhemko wenye nguvu. Katika ubeti wa 40, msimulizi anatumia sitiari ya ‘safina’ (chombo cha kusafiria majini) kurejelea sehemu ya siri ya Mwana Ninga. Katika ubeti wa 43, msimulizi anaeleza kuwa alihisi mawimbi ya maji yakisukumwa na upemo wa baharini kuelekea Manga (kwenye utukufu). Msimulizi anatumia sitiari hizi labda kutokana na uelewa wake wa shughuli za baharini na maeneo ya visiwa vya Lamu.

Vilevile, mandhari ya kijamii yanabainika katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Mandhari haya yanabainika kutokana na mahusiano mema ya kijamii yaliyomo. Katika beti za 1 – 6, msimulizi anawasihi watu wapige pembe kuwaita watu wengine wa karibu na hata wa mbali ili pamoja waweze kumsifu Mwana Ninga. Mandhari haya yanadokeza kuhusu uhusiano mwema mionganii mwa wanajamii katika mazingira husika. Vilevile, maudhui ya mapenzi baina ya msimulizi na mpenzi wake ni masuala ya mahusiano ya kijamii. Mandhari haya ya mapenzi yanaelekeza kwenye uhusiano mzuri baina ya wanawake na wanaume katika jamii hii. Masimulizi yanamulika kile ambacho wanajamii hawa wanakiona kuwa sifa za mwanamke mrembo.

Kuna mandhari ya msituni, msanii amemfananisha Mwana Ninga kama mti wa mgunga, pia kama ndege - Ninga.(ndege wa kuvutia).

Kuhusu mandhari ya kiwakati *Utendi wa Mwana Ninga* ilitungwa katika jadi ya Uswahlini hususan maeneo ya visiwa vya Lamu. Mandhari haya ya kiwakati yanaonekana kutokana na matumizi ya maneno mengi ya Kingozi ambayo ni lahaja ya zamani ya Kiswahili. Mashairi yaliyotungwa hivi karibuni hayana maneno mengi sana ya Kingozi.

Kimsingi, mandhari ya kijiografia ya *Utendi wa Mwana Ninga* ni katika maeneo ya visiwa vya Lamu na mandhari ya kibahari. Vilevile, *Utendi wa Mwana Ninga* una vielekezi vya mandhari ya Uarabuni kama vile vipodozi, vyombo vya mapambo na miti (mivije) au mimea.

## **4.2 WAHUSIKA KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

Wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni wawili. Wahusika hawa ni: Fumo Liyongo na Mwana Ninga.

### **4.2.1 FUMO LIYONGO**

Fumo Liyongo, ambaye pia ni mtunzi na msimulizi wa utendi huu anajitokeza kuwa mhusika mkuu. Fumo Liyongo ni mhusika wa kiume ambaye anamsifu mpenzi wake wa kike. Kabla ya kumwangazia Liyongo wa kimatini, tutamwangazia Liyongo wa kihistoria ambaye pia ni mtunzi wa utendi huu.

Mengi yamezungumzwa au kuandikwa kuhusu Fumo Liyongo wa kihistoria. Hata hivyo, kuna utata unaohusu tarehe ya kuishi kwa jagina huyu. Mulokozi (1999) akimnukuu Mulokozi na Sengo (1995) anaeleza kuwa Fumo Liyongo aliishi Pwani ya Kaskazini mwa Kenya kwenye maeneo ya Pate na Ozi katika karne ya kumi na tatu na baadaye. Kwa upande mwingine, Mulokozi anamnukuu Mbele (1989) akieleza kuwa Fumo Liyongo aliishi katika karne ya 9. Vilevile, Mulokozi anamnukuu Chiraghdin (1973) akieleza kuwa Fumo Liyongo aliishi katika karne ya 12 (baina ya miaka ya 1160-1204 M). Mulokozi anahitimisha kwa kusema kuwa tarehe inayoelekea kukubalika zaidi ni ile ya karne ya 13-14. Hii ni kwa kuwa Freeman-Grenville (1962) anaeleza kuwa katika kitabu cha *Tarekhe ya Pate*, mtawala wa eneo la Ozi aliitwa Fumo Liyongo na aliishi wakati wa utawala wa Fumo Omari, mtawala wa ki- Nabhany wa dola ya Pate miaka ya 1340-1393 M.

Mulokozi anaendelea kueleza kuwa Fumo Liyongo anasemekana kuwa mtoto wa mama masikini aliyeolewa katika familia ya kifalme ya Fumo. Fumo Liyongo alipendwa sana kwa kuwa alikuwa mwimbaji hodari, shujaa wa Waswahili, mchezaji ngoma na malenga wa ushairi. Fumo Liyongo

ametunga mashairi na nyimbo nyingi za arusi za kifalsafa na za kusifia mashujaa. Pia alitunga nyimbo kadha za kimapenzi za kumsifu mpenzi / mke wake. Miongoni mwa nyimbo hizi ni *Mwana Nazi, Wimbo wa Nazi na Mwana Mnga*. Mbali na usanii, Fumo Liyongo alikuwa mwindaji na mfanyibashara. Alifanya biashara katika sehemu za Pate. Yeye mwenyewe aliishi Ozi. Fumo Liyongo alisalitiwa na kuuawa na mwanaye na kisha akazikwa Ungwana wa Mashaha.

Japo *Utendi wa Mwana Ninga* unasemekana kuwa ilitungwa na Fumo Liyongo wa kihistoria, mwenyewe hajataja hili katika hitimisho kama ilivyo katika tenzi nyingine za Kiswahili za zamani. Bali ameuhitimisha utendi huu kwa kusifu nyayo za mpenzi wake *Mwana Ninga*.

Liyongo wa kimatini ambaye pia ni msimulizi wa utendi huu amejitokeza kama mhusika mwenye mapenzi makuu kwa mpenzi wake wa kike. Mapenzi yake yanajitokeza kupitia lugha nzito ya mahaba ambayo anatumia kumsifia mpenzi wake. Liyongo anajenga hisia za mapenzi miongoni mwa hadhira. Ni nadra kumpata mwanamume anayemsifu mkewe au mpenzi wake kwa kina na uwazi.

Liyongo pia anajitokeza kuwa mhusika aliye na uwezo na ujuzi mkuu wa kutumia lugha. Ubunifu wake wa kutumia tamathali za usemi hasa sitiari na jazanda anapozungumzia kuhusu tendo la ngono na mpenzi wake ni wa hali ya juu. Kupitia kwa matumizi ya tamathali hizi, Fumo Liyongo anafanikiwa kuibua picha halisi ya *Mwana Ninga*. Umuhimu wa Fumo Liyongo kama mhusika mkuu na pia msimulizi katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni kuendeleza maudhui ya sifa au wasifu. Kama tulivyoeleza, sifa zinazotolewa na mhusika huyu zinahusu urembo wa mpenzi wake *Mwana Ninga*. Hivyo, Fumo Liyongo anatuelekeza kwenye kile ambacho wanaume na vilevile jamii ya utungo huu inachokiona kuwa mwanamke mrembo.

Vilevile, Fumo Liyongo ndiye sauti ya usimulizi ya utendi huu. Sauti yake ni muhimu katika kuendeleza msuko wa hadithi hii. Pamoja na hayo, masuala ya mtazamo wa kijamii na mwonoulimwengu wao yanaendelezwa na mhusika huyu.

#### 4.2.2 MWANA NINGA

Mwana Ninga ni mhusika wa pili na mkuu katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika utendi huu, mhusika huyu amerejelewa kama: Mwananinga (ubeti wa 1), Yanga (ubeti wa 4) na Mwana Manga (ubeti wa 5- 6). Mwana Ninga ni mhusika wa kike na mpenzi wa Fumo Liyongo. Japo mhusika huyu hajitokezi mwenyewe na kutenda kama ilivyo katika tanzu za fasihi andishi, tunapata kumfahamu kupitia kwa sauti ya msimulizi.

Mwana Ninga amepewa sifa za mwanamke ambaye ni mrembo sana, mrefu na mwenye heshima. Sifa zake za urembo zimeelezwa na mtunzi kuanzia kichwani hadi nyayoni. Msimulizi anaeleza namna mwanamke huyu alivyo na nywele nzuri za singa kichwani. Kichwa chenyewe kinaleezwa kuwa kama marmar. Vilevile, masikio yake ni kama kombe la nanga. Uso umetengenea vizuri. Ncha za nyusi zake zinalingana na hazina mwanya wowote (zimepangika mfululizo). Msimulizi anaendelea kueleza zaidi kuwa nyusi zenyewe ni nyeusi kuliko wino. Midomo ya Mwana Ninga inaelezwa kuwa myembamba kiasi kwamba hata anaposema, mjinga ataelewa. Meno yake yanaelezwa kuwa yanameremeta na yanafanana na mwanga. Vilevile, Fumo Liyongo anaeleza kuwa ulimi wa Mwana Ninga ni mwepesi wa kusema au kunena.

Hali kadhalika, urembo wa Mwana Ninga kulingana na msimulizi wa *Utendi wa Mwana Ninga* unachangiwa na sifa zaidi za sehemu za mwili wake. Kidevu chake kinaleezwa kuwa shani (kisicho cha kawaida). Shingo yake ni ndefu kama ‘munga’ au ‘mugunga’ (mti mrefu wenye

miiba). Mabega yake ni kadri. Mikono na vidole vyake ni virefu. Kucha zake zina rangi ya kijani na yelete anayeziona bila shaka atatamani. Makwapa yake yanatoa harufu nzuri.

Msimulizi pia anaeleza kuhusu maziwa (matiti) ya Mwana Ninga ambayo anayalinganisha na matunda ya peponi. Kulingana na msimulizi, maziwa haya yanapokuwa yamefunikwa, yanashua macho na yanapokuwa yamefunuliwa, akili za yelete anayeyatazama zinaranda au kutanga (ubeti 32-33). Pamoja na hayo, mbavu za Mwana Ninga zinaleezwa kuwa laini kiasi cha kwamba yelete anaweza kuogopa kumpapasa kwa kuogopa kumdhuru. Vilevile, tumbo lake linaeleezwa kuwa lenye mikunjo na kitovu kizuri (ubeti wa 34-37).

Msimulizi anaendelea zaidi na kueleza kuhusu sehemu ya siri ya Mwana Ninga. Anaeleza kuwa sehemu hiyo (ambayo anaiita ‘safina’) si pana na pia si ndefu. Mtunzi anaeleza kisitiari na kijazanda namna alivyofurahia alipofanya mapenzi naye. Maelezo haya ya tendo la ngono yanalenga kuonyesha kuwa Mwana Ninga si mzuri au mrembo wa mwili tu bali pia mweledi katika tendo la ngono na kumtosheleza mpenzi wake kimapenzi.

Mtunzi amefanikiwa kuzieleza sehemu mbalimbali za mwili wa mpenzi wake huyu kama njia ya kudhihirisha urembo wake. Amefaulu kutumia lugha kwa usanii wa hali ya juu. Kutokana na maelezo haya, taswira kamili ya mwanamke huyu inanata akilini za hadhira au msomaji.

Katika utendi huu, Fumo Liyongo anaonyesha kuwa Mwana Ninga si mrembo wa mwili tu. Anaeleza kuwa hata ulimi wake ni mwepesi sana na hivyo ana ufasaha wa kusema na ni mwenye hekima. Liyongo anaeleza kuwa Mwana Ninga anapozungumza, hata mjinga humwelewa (ubeti wa 17).

Kimsingi, Mwana Ninga anasawiriwa kuwa mwanamke mrembo na wa kuvutia. Katika ubeti wa 31, Fumo Liyingo anaapa kuwa hajawahi kuona mwanamke mrembo kama Mwana Ninga.

Umuhimu wa mhusika Mwana Ninga ni kuwa ametumiwa kuendeleza maudhui ya mapenzi na urembo. Maelezo kuhusu urembo wake ndiyo yanayochukua sehemu kubwa ya masimulizi. Mwana Ninga ni muhimu sana katika kuendeleza masimulizi ya utendi huu. Bila yeye masimulizi haya hayawezi kutimia.

Mwana Ninga ni kiwakilishi cha mwanamke aliyetukuzwa. Msimulizi anatoa sifa nzuri, za urembo na ambazo zinampa fahari na mpenzi wake na hili ni jambo la kufurahisha mwanamke ye yote yule.

Mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu katika kuwasawiri wahusika wake. Amempa mwanamume nafasi ya kuonyesha kile ambacho anakiona kwa mwanamke mrembo. Kwa upande mwagine, mtunzi amempa mwanamke sifa nzuri ambazo zinachangia katika uumbaji wake. Uumbaji wa wahusika umeingiliana sana na kipengele cha usimulizi kwani msimulizi wa utendi huu ni mhusika mkuu katika utendi wenyewe. Sauti yake ni muhimu katika kuendeleza usimulizi. Hali kadhalika, uumbaji wa wahusika umeingiliana na kigezo cha mandhari na matumizi ya lugha katika utendi huu. Mtunzi amechota sitiari na tashibibi zake katika mandhari ya baharini na msituni, Us wahilini na Uarabuni. Mandhari haya yameendelezwa kuitia kwa lugha ya kitamathali. Miti, vyombo vyapambo na vyombo vyakusafiria ni vidokezo vyamandhari haya.

Vilevile, uumbaji wa wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga* umeingiliana na msuko wa utendi wenyewe. Kwa mfano, kueleza sifa za Mwana Ninga ni sawa na kueleza msuko wa utendi wenyewe.

Kufikia hapa tunaona kuwa mtunzi wa utendi huu amefanikiwa sio tu, katika usawiri wa wahusika, bali pia kuhakikisha kuwa kuna mwinglelano wa vipengele mbalimbali vyakifani

katika kuunda muundo mmoja wa utendi huu. Pia, usawiri wa wahusika umesaidia kuendeleza maudhui ya sifa ya mwanamke.

#### **4.3 HITIMISHO**

Katika sehemu hii, tumejadili mandhari na uumbaji wa wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeona kuwa *Utendi wa Mwana Ninga* una mandhari ya Uswahlini, Uarabuni na vilevile mandhari ya kibahari na ya msituni. Pia tumeona kuwa mandhari halisi ya kijamii yamechorwa. Kwa upande mwingine, tumeona kuwa wahusika ni wawili tu: Fumo liyongo ambaye ni msimulizi na Mwana Ninga ambaye ni mpenzi wake. Katika sura ifuatayo, tutajadili matumizi ya lugha, toni na usimulizi katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

## **SURA YA TANO**

### **MATUMIZI YA LUGHA, TONI NA USIMULIZI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

#### **5.0 UTANGULIZI**

Katika sura ya nne, tulihakiki usawiri wa mandhari na uumbaji wa wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika sura hii, tunahakiki matumizi ya lugha, toni na usimulizi katika utendi huu. Tunaanza na uhakiki wa matumizi ya lugha kisha toni na hatimaye usimulizi.

#### **5.1.0 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

Katika uhakiki wa matumizi ya lugha katika *Utendi wa Mwana Ninga*, tutazingatia viwango viwili vikuu. Viwango hivi ni uhuru wa kishairi na tamathali za usemi.

#### **5.1.1.0 UHURU WA KISHAIRI**

Katika sehemu hii, tunajadili uhuru wa kishairi wa kimsingi uliotumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

### **5.1.1.1 INKISARI**

Katika sura ya pili, tulieleza inkisari kama ufupishaji wa maneno katika shairi. Mbinu ya inkisari imetumika katika *Utendi wa Mwana Ninga* kwa wingi. Tutanukuu beti chache kutoka kwa utendi wenyewe kwa mifano:

Ubeti wa 3;

**Vumi lende mbali,**

**Lamshe ahali,**

Wake na wavuli,

waye nganga-nganga.

Katika ubeti huu, neno ‘lende’ katika mshororo wa kwanza ni inkisari ya kitenzi ‘liende’. Vilevile katika mshororo wa pili, kuna inkisari ‘lamshe’ badala ya ‘liamshe’. Mtunzi amefupisha silabi za kitenzi hiki kutokana silabi nne hadi tatu. Hatua hii imetusaidia kutosheleza kanuni ya idadi ya mizani sita katika kila ubeti.

ubeti wa 7;

**Takwanda kitwani,**

**Nduza sikiani,**

Hariri laini,

Zake nyele singa.

Sawa na ubeti wa tatu, ubeti wa saba hapo juu una inkisari mbili. ‘Takwanda’ yenyé mizani tatu badala ya ‘nitaanda’ yenyé mizani nne “nduza” ni ndugu zangu. Uamilifu wa inkisari hizi ni kuhakikisha kutimiza idadi ya mizani sita katika kila ubeti.

Inkisari katika utendi huu ni nyingi. Mifano zaidi inapatikana katika beti zifuatazo:

**Ubeti              Inkisari              kawaida**

11	lalofunga	lililofunga (mizani 5)
18	menoye	meno yake
18	takwambaye	nitakweleza kuhusu yeye
18	tatongoa	nitatongoa
24	shingoe	shingo yake
27	zandaze	zanda zake
28	napa	naapa
29	makwapae	makwapa yake
43	kwalina	kulikuwa na
51	nyaoze	nyayo zake.

Mifano hii inadhihirisha kuwepo kwa wingi wa inkisari katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Kama tulivyoeleza, jukumu kuu la inkisari katika utendi huu ni kutosheleza idadi ya mizani.

### **5.1.1.2 MAZIDA**

Tulieleza mazida kama mojawapo wa uhuru wa mshairi wa kurefusha neno kwa minajili ya kuongeza mizani katika neno hilo. Mbinu ya mazida hajatumika sana katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Ufuatayo ni mfano wa pekee tulioweza kuupata katika utendi huu.

Ubeti wa 40;

Yake safiina,

Nalipoiona,

Si nyire si pana,

Iyalie nyonga.

Katika ubeti wa 40, mtunzi ametumia neno ‘safiina’ lenye mizani minne badala ya ‘safina’, lenye mizani mitatu. Hivyo, msanii anatimiza kanuni ya idadi ya mizani sita katika kila mshororo. Hapa tunapata utata wa neno kwani ‘safiina’ (Lango la jehanamu) linaweza kiubua maana tofauti na muktadha huu wa kimapenzi.

### **5.1.1.3 TABDILA**

Tabdila ni hali ya kubadilisha mwendelezo wa neno bila kuongeza au kupunguza idadi ya mizani. Mbinu ya tabdila imetumiwa hapa na pale katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Zifuatazo ni baadhi ya beti ambapo mbinu hii imetumiwa.

Ubeti wa 7;

Takwanda kitani,

Nduza **sikiani**,

Hariri laini,

Zake **nyele** singa.

Ubeti wa 22;

Ulimi **mpesi**,

Wake ni fanusi,

Khasa kidurusi,

Hudighimu Yang'a.

Katika ubeti wa 7, kitenzi ‘sikieni’ linaendelezwa kama ‘sikiani’. Katika ubeti wa 22, kivumishi ‘mwepesi’ kinaendelezwa kama ‘mpesi’. Hatua hii ya kubadilisha mwendelezo ya maneno huwa na jukumu la kuvutia makini ya hadhira. Vilevile, mabadiliko hayo ni sehemu ya sajili ya ushairi.

#### **5.1.1.4.0 UHURU WA KIMSAMIATI**

Katika kundi hili tunajumuisha matumizi ya maneno au misamiati kutoka lugha, na lahaja nyinginezo za Kiswahili. Baadhi ya misamiati iliyotumiwa katika utendi huu imetolewa kutoka lugha ya Kiarabu na mingine kutoka lahaja ya Kingozi na Kiamu.

#### **5.1.1.4.1 MSAMIATI WA KIARABU**

Lugha ya Kiarabu imeathiri sana utunzi wa mashairi ya Kiswahili hasa ya zamani.

Katika mashairi mengi, maneno ya Kiarabu yametumika. Hali hii inaonekana pia katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

Baadhi ya maneno ya Kiarabu katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni:

Ahali- Watu (ubeti wa3)

Tuwakifu- tumalize (ubeti wa 6)

Ahamaru- -ekundu (ubeti wa 19)

Baiyani - bainika kuwa wazi (ubeti wa 33)

Kuwepo kwa misamiati ya Kiarabu katika utendi huu kunatokana maingiliano ya jamii hizi na kukopa kwa msamiati. Ni kutokana na sababu hii vilevile ndipo tunaona kuwa *Utenzi Mwana Ninga* pia anaitwa Mwana Manga – yaani, msichana kutoka Manga. Na katika ubeti wa 29 – 30, msimulizi anasimulia kuwa makwapa ya mpenzi wake yananukia kama mafuta ya kutoka Manga au Uarabuni. Hali kadhalika, katika ubeti wa 45, msimulizi anapoeleza kitendo cha kufanya mapenzi na Mwana Ninga, anaeleza kuwa alihisi ‘mawimbi ya maji yakisukuma kuelekea Manga’. Ni kutokana na kuwepo kwa misamiati ya Kiarabu katika *Utendi wa Mwana Ninga* ndipo tunaona kuwa mandhari ya utendi huu yana chembechembe za mandhari ya Uarabuni.

#### **5.1.1.4.2 MSAMIATI WA KINGOZI**

Kingozi ni lahaja ya zamani ya Kiswahili. Tenzi nyingi za Kiswahili na hata mashairi ya kisasa yana misamiati ya Kingozi. Tunatoa mifano michache katika *Utendi wa Mwana Ninga* kudhihirisha hoja hii:

<b>Ubeti</b>	<b>Kingozi</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>
2	uambe	useme
8	enga	angalia / tazama
13	kuyenga	kuangalia
18	takwambaye	nitakueleza kuhusu yeye
32	siwenepo	sijaonapo.

Matumizi ya Kingozi huchukuliwa kuwa kitambulishi cha sajili ya ushairi. Vilevile, kuwepo kwa msamiati wa Kingozi katika utendi huu kunatokana na sababu kuwa Kingozi ni mionganoni mwa lahaja za Kiswahili zilizokuwa zikitumika wakati wa utunzi wa utendi huu.

#### **5.1.1.4.3 MSAMIATI WA KIAMU**

Lahaja ya Kiamu huzungumzwa mjini Lamu. *Utendi wa Mwana Ninga* umetungwa katika lahaja ya Kiamu. Ni kutokana na sababu hii ndipo tunaona kuwa msamiati wa Kiamu ni mwingi mno. Mifano ya msamiati wa Kiamu katika utendi huu ni kama ifuatayo:

<b>Ubeti</b>	<b>Kiamu</b>	<b>Kiswahili sanifu</b>
1	pijiani	pigeni
2	upije	upige
3	waye	waje
7	kitwani	kichwani
7	nyele	nywele
9	mashikio	masikio
17	miomo	midomo
20	wanda	wanja
23	kievu	kidevu
24	mwandi	mwanzi

Kutoka kwa mifano tuliyoinkuu hapo juu, tunaona kuwa katika Kiamu na lahaja zingine za kaskazini, sauti ‘j’ hutumiwa badala ya ‘g’ kama vile katika ‘upije’ na ‘upige’ sauti ‘t’ hutumiwa badala ya sauti ‘ch’ kama vile katika ‘kitani’ na ‘kichwani’. Sauti ‘d’ hutumiwa badala ya sauti ‘j’ kama vile katika ‘wanda’ na ‘wanja’. Sauti ‘d’ hudondoshwa inapotokea baina ya irabu ‘i’ na ‘o’ au ‘i’ na ‘e’ kama vile katika ‘miomo’ badala ya ‘midomo’ na ‘kievu’ badala ya ‘kidevu’.

Msamiati wa Kiamu katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni mwingi na hatuwezi kuujadili na kuumaliza. Kimsingi, kuwepo kwa wingi wa misamiati hii kunatuelekeza kwa mazingira ya

kijiografia ambako utendi huu ultungiwa. Ni kutokana na hali hii ndipo tulieleza kuwa *Utendi wa Mwana Ninga* umetungwa katika lahaja ya Kiamu na kuwa mandhari yake ni maeneo ya visiwa vya Lamu. Hivyo, matumizi ya lugha yanaingiliana na kukamilishana na ujenzi wa mandhari.

#### **5.1.1.4.4 UHURU WA KISINTAKSIA KATIKA *UTENDI WA MWANA NINGA***

Tunapozungumza kuhusu uhuru wa kisintaksia katika matumizi ya lugha, huwa tuna maana ya kutofuata miundo ya sentensi, vishazi na virai kwa mujibu wa kaida za lugha husika. Uhuru wa kisintaksia pia hujulikana kama kuboronga sarufi au mpinduo wa sintaksia.

Mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* ametumia mpinduo wa sarufi katika sehemu mbalimbali za utendi huu. Baadhi ya sehemu hizi ni katika beti zifuatazo:

Ubeti wa 6;      **Basi tuwakifu,**

**Yasiwe marefu,**

**Sifa tusanifu,**

**Zake Mwana Ninga.**

Ubeti wa 9;      **yake mashikio,**

**Apulikiao,**

**Yatendele tao,**

**Kama kombe nanga.**

Ubeti wa 40;      **Yake safiina,**

Nalipoiona!

Si nyire si pana,

Iyalie nyonga.

Katika ubeti wa 6, mtunzi anasema ‘sifa tusanifu’ badala ya ‘tusanifu sifa’. Katika mfano huu, mtunzi anakiuka kaida ya kisarufi ya nomino kuja baada ya kitenzi. Pia katika ubeti wa 9 na wa 40; mtunzi anakiuka kaida ya kivumishi kuja baada ya nomino. Kisarufi, tunatarajia kwa mfano kupata katika ubeti wa 40, mshororo wa kwanza mtunzi akisema ‘safiina yake’.

Mpinduo wa kisintaksia huwa ni kitambulisho cha rejista ya ushairi. Vilevile, huwa ni dhihirisho la uwezo wa msanii wa kujitokeza ma miundo tofauti ya kisintaksia na hivyo kuwa amemakinika katika lugha husika. Pamoja na hayo, ukiushi wa kisintaksia huwa na uamilifu wa kuongeza ladha au uzuri katika ushairi, kama tulivoona katika utendi huu tunaoshughulikia.

#### **5.1.2.0 TAMATHALI ZA USEMI**

Katika sura ya pili tumeeleza tamathali za usemi kuwa aina ya ukiushi katika matumizi ya lugha ambapo muundo wa lugha na vilevile maana ya kimsingi ya maneno hukiukwa. Katika sehemu hii, tunahakiki tamathali ambazo zimetumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Aidha hiki ni kipengele cha nadharia ya U mundo na kinaangalia muundo wa ndani wa utendi huu.

### **5.1.2.1 SITIARI**

Sitiari ni tamathali ambayo ni muhimu sana mionganoni mwa tamathali za usemi. *Utendi wa Mwana Ninga* umetumia sitiari mbalimbali.

Katika utendi huu, Fumo Liyongo anamwita mpenzi wake ‘Mwana Munga’. ‘Munga’ au ‘mugunga’ ni aina ya mti mgumu sana, wenge miba. Hatua ya kumwita mhusika huyu ‘Munga’ inadhamiriwa kuonyesha kuwa yeye ni mwanamke ambaye ni mgumu na thabiti katika mienendo yake na kamwe hawezi kufikiwa na mwanamume yejote kwa urahisi. Tabia zake ni za kipekee. Miiba ya mti huu inashiria kwamba tabia njema ya msichana huyo ni kinga imara dhidi ya wanaume ambao huenda wakamtaka kimapenzi. Urefu wa mti wa mgunga pia ni sifa ya kuweza kukinga majani yake yasifikasiwe na wanyama waharibifu. Ni twiga tu ambaye ana uwezo wa kuyafikia majani hayo mionganoni mwa wanyama wala majani. Sifa hii pia inaonyesha kuwa mwanamke huyu hawezi kufikiwa na wanaume kiholela ila mmoja tu – mpenzi wake Fumo Liyongo.

Sitiari ya ‘munga’ au ‘mugunga’ inaendelezwa katika beti zaidi za *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika ubeti wa 27, vidole vya Mwana Ninga vinaelezwa kuwa ‘matanzu ya mnga’. Sawa na mnga wenye, tanzu zake huwa ndefu. Hivyo, sifa ya urefu wa Mwana Ninga katika sehemu zake zote za mwili inaendelezwa kusisitiza urembo wake.

Vilevile jina la mhusika huyu ‘Ninga’ limetumiwa kisitiari. TUKI (1981:215) wanaeleza ‘Ninga’ kuwa “ndege wa jamii ya tetere mwenye rangi ya kijani na miguu myekundu, hupenda kula kuyu, kunazi na mbono”. Ninga anajulikana kuwa ndege wa kifahari, mwenye rangi za kuvutia na sauti nzuri. Sifa za urembo wa ninga zinatumwiwa kumsawiri mpenzi wa Liyongo kuwa mrembo wa kuvutia. Hali kadhalika, ndege ninga huishi katika kilele cha mti wa mkuyu,

mkunazi au mbono na hivyo vigumu kumpata au kumkamata kwani ni nadra kwake kukanyaga chini. Hivyo huonekana tu na kutamaniwa kwa mbali. Mtunzi anaendelea tu kuashiria kuwa Mwana Ninga ataendelea tu kutamaniwa na wanaume wengine ambaeo hawana uwezo wa kumfikia.

Katika ubeti wa 24, shingo ya Mwana Ninga inasemekana kuwa mwanzi. TUKI (1981:203) wanaeleza mwanzi kuwa ‘mti unaofanana na mau au hinzirani wenyewe uwazi ndani kama mrija’. Kutohakana na maelezo haya, tunabaini kuwa sifa ya urefu wa Mwana Ninga inasisitizwa. Hali hii inaonyesha mtazamo wa msimulizi kuwa mwanamke mrefu mwembamba ndiye mrembo zaidi.

Sitiari nyingine katika *Utendi wa Mwana Ninga* imetumika katika ubeti wa 40. Katika ubeti huu, sehemu ya siri ya Mwana Ninga inarejelewa kama ‘safina’. Safina ni chombo cha kusafiria baharini. Hatua ya msimulizi kuiita sehemu ya siri ‘safina’ inaonyesha umuhimu wa sehemu hii kwa msimulizi. Katika mazingara ya bahari, chombo cha kusafiria majini ni muhimu sana kwa wakazi wa mazingara haya kwa kuwa kinawezesha kuendelea na shughuli zao za uvuvi, biashara na usafiri. Wakazi wa baharini hawawezi kumudu maisha yao kwa urahisi bila vyombo vya kusafiri majini. Pamoja na hayo, msimulizi katika ubeti wa 43, ametumia ‘mawingu’ na ‘upepo’ kisitiari kurejelea zile hisia za nguvu zinazompata msimulizi anapofanya mapenzi na mpenzi wake. Vilevile, msimulizi katika ubeti wa 43 anatumia sitiari ya ‘vyombo’.

Ubeti 43;            **kwalina mawingu,**

Na pepo nyengwangu,

zote zombo zangu,

kazifungafunga.

Katika ubeti huu, ‘zombo’ au ‘vyombo’ ni sitiari inayotumiwa kitasifida kurejelea sehemu za siri za msimulizi.

Sitiari ya ‘ndiwa’ imetumiwa katika ubeti wa 48. Msimulizi anatumia sitiari hii kumrejela mpenzi wake. Njiwa ni ndege ambaye anajulikana kuwa mwerevu na mpole. Ndege huyu hufugwa nyumbani na huaminiwa kuwa mwenye baraka au bahati nzuri. Njiwa pia huwa na rangi za kupendeza ambazo huwafanya kuonekana warembo zaidi. Kurejelea Mwana Ninga kama njiwa kunachangia katika maudhui ya sifa za mwanamke. Mwana Ninga, na kwa kiwango cha juu, mwanamke anapewa hadhi.

Kimsingi, sitiari zilizotumika ni za mimea, ndege na hali ya baharini. Sitiari hizi zimesaidia kaitka usawiri wa wahusika. Kutokana na hali hii, kuna mwingiliano mkubwa baina ya vipengele hivi vya kifani na maudhui ya utendi huu.

#### **5.1.2.2 TASHIBIHI**

Sawa na sitiari, tashibihi ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja na kingine. Hata hivyo, tofauti na sitiari, tashibihi huwa ni ulinganishaji wa kutumia maneno ya kiulinganishi. Tashibihi zimetumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga* kwa wingi kuliko tamathali nyingine yoyote. Mbinu hii imetumiwa kulinganisha sehemu mbalimbali za mwili wa Mwana Ninga na vitu mbalimbali. Tutatoa mifano kuonyesha hali hii.

Katika ubeti wa 8, msimulizi anaeleza kuwa kichwa cha Mwana Ninga ni kama rukhamu (marmar). TUKI (1981:154) wanaeleza ‘marmar’ au ‘marumaru’ kuwa namna ya jiwe liwezalo kung’arishwa vizuri, hutumika kuwa pambo la kuta za nyumba na sakafu. Jiwe hili la tunu ni

nadra kupatikana. Tashibihi hii inaonyesha uzuri wa kichwa cha Mwana Ninga, uzuri ambao msimulizi anaona kuwa tunu kwake. Pamoja na kichwa, msimulizi anaeleza katika ubeti wa 9 kuwa masikio ya Mwana Ninga ni kama kombe la nanga. Hali hii inaashiria kuwa masikio hayo yamepinda vizuri na yana ushupavu wa kusikiliza, kusikia na kuelewa.

Tashibihi nyingine inatumika katika ubeti wa 12 wa *Utendi wa Mwana Ninga*. Katika ubeti huu, nyusi za Mwana Ninga zinaelezwa kuwa nyeusi mno zaidi ya wino. Kupitia kwa tashibihi hii, msimulizi anaendelea kumsifu mpenzi wake kwa kuonyesha weusi wa nyusi zake.

Hali kadhalika, meno ya Mwana Ninga yanaelezwa kuwa meupe na yanayofanana na mwanga ung'ao Uarabuni (Manga);

Ubeti wa 19;

Si ya akhadharu,

Si ya ahamaru,

Hufana na nuru,

Iwaa Manga.

Kulinganisha meno ya Mwana Ninga na mwanga ung'ao katika Manga kunaelekeza kwa imani ya msimulizi kuwa chochote kitokacho Manga ni kizuri.

Katika ubeti wa 22, tunapata tashibihi ‘ulimi wake ni mwelesi, ni kama fanusi’. Tashibihi hii inalinganisha welesi wa ulimi wa Mwana Ninga na fanusi au kibatali (taa ya kikopo). Kibatali huwa na welesi wa kuwashwa na vilevile kuzimka au kuzimwa. Tashibihi hii ni muhimu katika mawasiliano. Katika ubeti huu, msimulizi anaeleza kuwa Mwana Ninga anapozungumza, sauti yake hufanya angani kama mwangwi’. Husikika kwa njia wazi ya kupendeza.

Tashibihi zaidi katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni kama zifuatazo: Shingo yake ni ndefu kama mwanzi mkubwa (ubeti wa 24), Mafuzi (mabega) yake ni kadri kama bilauri (ubeti wa 26), vidole vyake ni virefu kama tanzu za munga (ubeti wa 27), kucha zake zina rangi kama marijani (ubeti wa 28).

Kimsingi, tashibihi zinazotumika katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni nyingi. Tashibihi hizi zina uamilifu wa kumsawiri mhusika Mwana Ninga na kudokeza kuhusu mandhari ya utendi wenyewe.

### 5.1.2.3 CHUKU

Chuku ni hali ya kutia chumvi katika usemi. Chuku huwa mbinu muhimu katika tungo za kiwasifu kama vile *Utendi wa Mwana Ninga*.

Chuku katika Utendi wa Mwana Ninga imetumiwa kama msingi wa kusawiri watusika na sifa zao. Maeleo kuhusu sifa za Mwana Ninga yanetiwa chumvi.

Kwa mfano, katika ubeti wa 8, kichwa cha Mwana Ninga kinalinganishwa na rukhamu (marmar). Tulieleza marmar kama aina ya jiwe la tunu na litumiwalo kung'arisha kuta za nyumba. Kulinganisha kichwa cha binadamu na jiwe la thamani ni chuku. Chuku hii inatumiwa kama njia ya kuonyesha sifa ya kung'ara kwa Mwana Ninga. Haiwezekani mtu kung'ara mithili ya madini. Vilevile katika ubeti wa 9, masikio ya Mwana Ninga yanaelezwa kuwa yametanda kama kombe la nanga. Kombe la nanga ni kubwa mno na kamwe hakuna mwanadamu aliye na masikio makubwa au yaliyotanda kama hayo.

Chuku pia inajitokeza katika ubeti wa 12:

(Nyusi) Ni nyeusi mno,  
Zaidi ya wino,  
Zitwalie kono,  
Ya tandu za manga.

Katika mshororo wa kwanza na pili, msimulizi anaeleza nyusi za Mwana Ninga ni nyeusi mno zaidi ya wino (mweusi) na ndefu sana kama matawi ya manga. Bila shaka maneno haya yametiwa chumvi ili kuonyesha urembo wa Mwana Ninga.

Katika ubeti wa 13, msimulizi anatumia chuku anaposema kuwa Mwana Ninga afumbapo macho na kisha kuyafumbua, hushtua kila anayemtazama. Vilevile, pua yake inaelezwa kuwa ya ajabu kwa kuwa ina mikunjo sita. Zitefute (mifupa ya mashavu) zake zinaelezwu kuwa zimeshinda zote kwani ni za mafuta yaliyosafishwa (ubeti wa 16). Haiwezekani kuwa msimulizi ameziona zitefute za watu wote ulimwenguni na kuzilinganisha na za Mwana Ninga kabla ya kuamua kuwa hivyo ni bora zaidi.

Chuku nyingine ipo katika ubeti wa 17. Msimulizi anaeleza kuwa Mwana Ninga anaposema, hata mjinga anamwelewa. Hii yaelekea kuwa kinaya pia. Chuku hii inaashiria kuwa Mwana Ninga ni mjuzi wa kusema na vilevile mwenye maarifa. Hii ni chuku kwa kuwa mtu mjinga ni mjinga tu hata aseme nani, hataelewa. Hali kadhalika, meno ya Mwana Ninga yanaelezwa kuwa yanayong'ara na kutoa mwanga ung'ao katika Manga (Uarabuni). Maeleo haya pia ni chuku ambayo inalenga kuendeleza maudhui ya sifa. Vilevile, chuku hii inaonyesha imani ya msimulizi kuwa chochote kitokacho Manga (Uarabuni) ni kizuri.

Katika beti za 21 na 22, kinywa cha Mwana Ninga kinapewa maelezo ya chuku. Kinywa chake kinasemekana kuwa kinarudisha mivuke kila mara anapozungumza. Vilevile, ulimi wake unaelezwa kuwa mwelesi kama fanusi (kibatali) na kila asemapo neno, mwangwi husikika angani. Katika hali ya kawaida haiwezekani kuwepo mtu ambaye kila anapotamka neno moja, mwangwi usikike angani. Chuku hii ina lengo la kuendeleza sifa za kiusemi za Mwana Ninga.

Hali kadhalika, shingo ya Mwana Ninga inaelezwa kuwa ndefu kama mwanzi mkubwa (ubeti 24). Hali hii inaonyesha kuwa msimulizi anathamini sana mti huu wa mwanzi na hivyo anaonelea kuwa chochote kizuri kinafaa kuwa na sifa za mwanzi. Chuku hii pia inaendelezwa katika ubeti wa 27 ambapo msimulizi anaeleza kuwa mikono ya Mwana Ninga ni mirefu na vidole vyake vinaning'inia kama tanzu za mnga.

Katika ubeti wa 30, msimulizi anaeleza kuwa makwapa ya Mwana Ninga yanapendeza kuyaona na yanatoa harufu nzuri zaidi ya ua la asumini au mafuta matukufu kutoka Manga. Hii haiwezekani kwani makwapa hutoa harufu ya jasho isiyovutia.

Chuku zaidi imetumiwa katika ubeti wa 34 ambapo mtunzi anaeleza kuwa mbavu za Mwana Ninga ni laini kiasi kwamba zinaogofya yejote anayemsinga au kumkanda na kumfanya atahadhari ili asije akamdhuru. Vilevile, katika ubeti wa 37, msimulizi anaeleza kuwa kitovu cha Mwana Ninga si cha kawaida. Ni kikubwa mfano wa huka (kijaluba) na kuwa mwenye kumnusa huwa na uchepechepe wa damu puanī mwake. Bila shaka, ni kinyume cha hali ya kihalisi mtu kupata chembechembe za damu puanī kutokana na kuinusa sehemu yoyote ya mwili wa mwanadamu.

Kilele cha matumizi ya chuku katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni katika beti za 40 – 47 ambapo mtunzi anasimulia namna alivyofanya mapenzi na Mwana Ninga. Kwa kutumia lugha ya

kitamathali, mtunzi anatia chumvi katika uwezo wao katika shughuli hiyo, na kwamba baada ya kushusha, mtunzi alitetemeka kama mgonjwa ambaye waganga wameshindwa kumtibu (ubeti 47).

Kufikia hapa, tumeona mifano ya chuku katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Msimulizi amefanikiwa kutumia chuku nyingi kama ilivyo katika tungo za kiwasifu. Vilevile, chuku alizotumia zimeleuliwa kwa usanii wa hali ya juu kwani zimeoana vizuri na mandhari ya utendi huu. Pia chuku hizo zimeendeleza madhumuni ya sifa.

#### **5.1.2.4 USAMBAMBA**

Ingawa usambamba upo wa aina nyingi, usambamba tunaozingatia katika sehemu hii ni usambamba wa kimuundo na wa kifahiwa. Usambamba wa kimuundo unahuksu kurudiwa kwa muundo fulani wa kisintaksia katika utungo. Kwa upande mwingine, usambamba wa kifahiwa unahuksu kurudiwa kwa neno lile lile au matumizi ya kisawe cha neno hilo katika utungo fulani.

Usambamba wa kimuundo umetokea katika beti za 5 na 6.

Ubeti 5; Kisa kuziona,

Baiti kufana,

Yatupe kunena,

**Zake Mwana Manga.**

Ubeti 6; Basi tuwakifu,

Yasiwe marefu,

Sifa tusanifu,

**Zake Mwana Manga.**

Usambamba mwingine upo katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa 32 na 42; **Yake Mwana Manga.**

#### **5.1.2.5 TASHIHISI**

Mbinu ya tashihisi hajatumika kwa wingi katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Mfano wa pekee unapatikana katika ubeti wa 3.

Ubeti 3; **Vumi lenda mbali,**

**lamshe ahali,**

wake na wavuli,

waye nganga-nganga.

Fumo Liyongo anawataka watu wapige pembe ili ‘ujumbe uende mbali uwaamshe watu’ ili waje wamsaidie kumsifu mpenzi wake. (Vumi) sauti inayotoka kwenye pembe imehuishwa kwani imepewa sifa ya uhai ya kuweza ‘kwenda’ na vilevile uwezo wa ‘kuwaamsha’ watu. Tashihisi hii inaonyesha namna pembe ya nyati inavyoweza kutoa sauti kubwa yenye uwezo mkuu.

### **5.1.2.6 NIDAA**

Katika sura ya pili, tulieleza nidaa kama mbinu ya kutumia maneno ya kuibua hisia. Maneno hayo hutumiwa mara nyingi pamoja na alama hisi (!).

Mbinu ya nidaa imetumiwa katika ubeti wa 40.

Yake safiina,

Nalipoiona!

Si nyire si pana,

Iyalie nyonga.

Katika ubeti wa 40 hapo juu, kitenzi ‘nalipoiona!’ kimetuika kwa njia inayoweza kuibua hisia za matamano mionganini mwa hadhira. Msimulizi anaeleza namna alivyoiona sehemu ya siri ya mpenzi wake ambavyo si ndefu na si pana. Matumizi ya alama hisi (!) yananuiwa kuonyesha namna msimulizi alivyostaajabu na vilevile kuvutiwa na uzuri au urembo wa mpenzi wake. Beti zinazofuatia ubeti huu wa 40, na ambazo zinaeleza kuhusu kitendo cha ngono baina ya msimulizi na mpenzi wake vilevile zimetumia maneno ya kuibua hisia za matamano na hamu ya mapenzi.

### **5.1.2.7 TASIFIDA**

Mbinu ya tasifida imetumiwa na mtunzi kurejelea sehemu za siri au za uzazi. Tasifida imetumika kupitia kwa tamathali nyingine za lugha. Mfano wa mbinu hii unapatikana katika ubeti wa 32:

Napa siwenepo,  
Sishuhudiepo,  
Matunda ya pepo,  
Yake Mwana Manga.

Katika ubeti wa 32 hapo juu, msimulizi anatumia sitiari ya ‘matunda ya pepo’ kurejelea matiti ya Mwana Ninga. Msimulizi anaona haya au soni kutaja ‘matiti’ hasa anaposimulia kuhusu mpenzi wake. Ni kama msimulizi anaona kuwa atakuwa anamkosea mpenzi wake nidhamu iwapo ataamua kutumia lugha wazi. Hivyo, mtunzi anataka kudhihirisha namna anavyompenda, au kumthamini na kumheshimu mpenzi wake.

Vilevile katika ubeti wa 40, msimulizi ametumia sitiari ya ‘safina’ kama njia ya matumizi ya tasifida. Neno ‘safiina’ limetumiwa kurejelea sehemu ya siri ya Mwana Ninga. Msimulizi ameona soni kutumia jina la moja kwa moja au lugha ya kawaida ili kudumisha adabu. Msimulizi amedhihirisha heshima kwa mpenzi wake. Pamoja na hayo, msimulizi ametumia misamiati ya baharini kisitiari kurejelea hali yakufanya mapenzi na Mwana Ninga. Msimulizi anatumia misamiati kama vile ‘ngamani’ (ubeti 41) kurejelea ndani ya sehemu ya siri, ‘vyombo’ (ubeti 43) kurejelea sehemu za kiume, ‘piga mzinga’ (kutoa shahawa) na kadhalika. Athari za lugha hii ya kisitiari ni kuwa imeficha aibu na kumwezesha msimulizi kudhihirisha heshima zake kwa mpenzi wake na hadhira. Pia tasifida imesaidia kuonyesha ubunifu wa mtunzi katika matumizi ya lugha na uchoraji wa mandhari ya kibahari.

### **5.1.2.8.0 TAKRIRI**

Ni mbinu ya kisauti ya kurudia irabu, konsonanti au silabi au neno katika utungo fulani.

#### **5.1.2.8.1 TAKRIRI IRABU**

Ni hali ya kurudia irabu ileile katika sehemu sawia za neno katika sentensi. Mfano unapatikana katika beti zifuatazo za *Utendi wa Mwana Ninga*:

Ubeti 13;      Mato avikapo,

Khasa avuapo,

Mtu akiwepo,

Hutisha kuyenga.

ubeti 17;      Miomo nyembamba,

Asipoifumba,

Atakapokwamba,

Helewa muinga.

Athari ya takriri irabu ni kuleta wizani / ridhimu katika utungo wa kifashi hasa katika ushairi.

### **5.1.2.8.2 TAKRIRI KONSONANTI.**

Takriri konsonanti ni kurudia konsonanti ileile katika neno au maneno katika mshororo au ubeti.

Mifano:

Ubeti 42;      **Ikimekameka,**

**Ikinukanuka**

**Vumba la kimaka,**

**Yake Mwana Ninga.**

Katika ushairi wa Kiswahili, takriri irabu na takriri konsonanti hazijitokezi sana kama katika

Kiingereza kwani Kiswahili hupendelea muundo wa konsonanti kufuatwa na irabu.

### **5.1.2.8.3 TAKRIRI SILABI**

Takriri silabi ndiyo aina ya urudiaji ambao unapatikana kwa wingi katika tungo za kishairi.

Silabi zinazorudiwa mara nyingi huwa muungano wa konsonanti na vokali. Takriri silabi imetumiwa katika vina vya mishororo ya kila ubeti. Vina vya mishororo ya kwanza mitatu vinarudiwa rudiwa. Tunanukuu ubeti wa 37 kama mfano:

**Kitovu ni huka,**

**Kezo la kimaka,**

**Mwenyi kumnuka,**

**Pua damu henga.**

Katika ubeti wa 37 hapo juu, kina ‘ka’ kinarudiwa katika mishororo tatu.

Vilevile, kina cha mshororo wa mwisho wa kila ubeti kinarudiwarudiwa katika mishororo yote ya mwisho katika utendi mzima. Kina hiki ndicho kinachoufanya utendi kuwa na bahari. Tenzi zote huwa na bahari kama mojawapo wa kaida za utunzi wa tenzi. Bahari ya utendi huu ni ‘nga’.

Mbali na takriri zinazohusu vina, kuna takriri ambazo pia zinahusu silabi za kuanzia mishororo ya beti. Baadhi ya beti katika *Utendi wa Mwana Ninga* zina takriri ya aina hii. Mifano:

Ubeti 32;      **Napa siwenepo,**  
                     **Sishuhudiepo,**  
                     **Matunda ya pepo,**  
                     **Yake Mwana Manga.**

Ubeti 34;      **Ziwavuze mwana,**  
                     **Ziwavu zinana,**  
                     **Hutisha kuvina,**  
                     **Wenyi kumsinga.**

#### **5.1.2.8.4 TAKRIRI NENO**

Huu ni urudiaji wa neno ili kuleta msisitizo fulani

Ubeti 23:      **Kungu-kungu Manga**

Ubeti 42:      **Ikimekemeka, ikinukanuka**

Ubeti 43:      **Kazifungafunga**

Takriri huwa na jukumu la kuleta wizani katika utungo wa kifasihi. Wizani huo huwa na uwezo wa kufanya kazi ya kisanaa kuwa ya kuvutia. Kwa jumla, mtunzi wa utendi huu amefaulu katika matumizi ya mbinu ya takriri na hivyo kuufanya utungo huu kuwa wa kuvutia.

## **5.2 TONI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

Katika sura ya pili, tulieleza toni kuwa mtazamo au mkabala anaouchukua mtunzi kuhusu wahusika wake, mandhari, hali au masuala anayoyazungumzia.

*Utendi wa Mwana Ninga* unadhihirisha toni ya mapenzi au mahaba. Lugha ya mahaba ambayo inaonyesha hisia za mapenzi ya msimulizi kwa Mwana Ninga. Mtunzi ametoa sifa za mpenzi wake ambazo zinahusu urembo wa kimwili. Urembo huu unahusiana moja kwa moja na mapenzi kwa kuwa nyingi ya sehemu anazozitaja ni zile za kuweza kuibua ashiki au msisimko wa mapenzi. Kwa mfano, anataja kuhusu nywele laini za singa (ubeti wa 7), uso mzuri wa kuvutia (ubeti wa 10), nyusi nyeusi zinazolingana na kufungamana (ubeti 11), macho ya kutisha (ubeti 13), midomo myembamba (ubeti 17), meno yang'aayo (ubeti 19), kidevu cha shani (ubeti 23), shingo ndefu (ubeti 24), mabega ya kadri (ubeti 26), makwapa yenyе harufu nzuri (ubeti 29), matiti mazuri (ubeti 32), mbavu nyembamba (34), kitovu kama kijalabu (ubeti 37), sehemu za siri za kadri (ubeti 40), magoti ya kuviringa (ubeti 49) na kadhalika. Hali hii ya kusimulia kuhusu sehemu hizi inaonyesha toni ya mapenzi.

Toni ya mapenzi imechanganyika na toni ya kutosheka. Msimulizi ameapa na kukariri mara kadha kuwa hajaona mwengine mrembo kama Mwana Ninga (ubeti 31, 32). Hali hii inaonyesha kuwa msimulizi ametosheka na kuridhika na kuwa na Mwana Ninga kama mpenzi

wake. Hali hii pia inaonyesha imani ya mtunzi kuwa hakuna mwingine mrembo kama au kushinda Mwana Ninga.

Msimulizi pia amedhihirisha toni ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Kupitia ubeti wa 15, mtunzi anatuelekeza kuamini kuwa Mungu ndiye aliyemuumba Mwana Ninga na kumpa uzuri wote alionao. Anasimulia kuwa Mungu anao uwezo wa kufanya mikunjo hata ishirini kwa pua kama namna alivyotengeneza mikunjo sita kwenye pua ya Mwana Ninga. Hivyo, msimulizi anaonyesha toni ya kuamini Mungu na kuridhika na yale anayotengeneza au kutupa, ni ya kuridhisha.

Masimulizi pia yanadhihirisha imani kuwa chochote kizuri kinatoka Manga. Imani hii imebainika kupitia kwa namna au jinsi msimulizi anavyoteua baadhi ya tamathali zake. Kwa mfano, mtunzi ameteua sitiari na tashibibi za kiulinganishi sifa za Mwana Ninga na vitu au vyombo mbalimbali kutoka Manga (Uarabuni). Kwa mfano, katika ubeti wa 19, msimulizi analinganisha kung'ara kwa meno ya Mwana Ninga na mwanga ambao unang'aa katika Manga (Uarabuni). Hali kadhalika, katika ubeti wa 45, msimulizi anaeleza kuwa alipofanya mapenzi na Mwana Ninga alihisi 'mkondo wa maji yanayokwenda Manga'. Kurudiarudia kutaja 'Manga' kunaelekeza kwa mtazamo wa kiimani wa msimulizi kuwa chochote kizuri kinatoka Manga au Uarabuni.

Toni ya uaminifu pia imejitokeza katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Hali ya msimulizi kumsifia mpenzi wake, na kuapa kuwa hakuna mwengine mrembo kama ye ye kunaonyesha uhusiano mwema baina ya msimulizi na mpenzi wake. Msimulizi anadhihirisha uaminifu wake kwa mpenzi wake, hawezi kumsaliti kwa kusifia mwanamke mwingine. Toni hii ina uwezo wa

kuathiri hadhira na kuwapa mwelekeo wa kutaka kuwasifu wapenzi wao. Vilevile, toni hii ina uwezo wa kuibua hisia za wivu mionganini mwa hadhira.

Kwa ujumla, toni ya mapenzi, uhusiano mwema, imani na uaminifu imejitokeza katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Toni hii imetokana zaidi na matumizi ya lugha ya kitamathali. Pia toni hii imetokana na usawiri wa wahusika, mandhari na maudhui au yaliyomo. Vipengele hivi vya fani vinaingiliana na kukamilishana.

### **5.3 USIMULIZI KATIKA UTENDI WA MWANA NINGA**

Usimulizi ni mojawapo wa vipengele muhimu na vipana vya kifani. Kwa sababu ya muda, hatutaweza kujadili kipengele hiki kwa undani ila tutazingatia masuala ya kimsingi ya usimulizi.

*Utendi wa Mwana Ninga* una mseto wa mbinu za kisimulizi. Kuna mchanganyiko wa vitambulishi vya nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja.

Nafsi ya kwanza umoja huwakilishwa na kiwakilishi ‘mimi’ pamoja na kiambishi kiwakilishi ‘ni’ katika vitenzi. Kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja hurejelea mtunzi ambaye pia huchukua nafasi ya msimulizi katika kazi ya fasihi. Msimulizi wa aina hii pia huwa mhusika katika kazi husika. Katika *Utendi wa Mwana Ninga*, Fumo Liyingo anasimulia yeye mwenyewe kuhusu sifa za mpenzi wake. Kwa hali hii, Fumo Liyongo ni msimulizi na pia mhusika. Hivyo, yeye ndiye nafsi ya kwanza umoja. Katika utenzi wote, Fumo Liyongo anajirejelea katika ubeti wa 31, anasema ‘Naapa wallahi ...’. Katika ubeti wa 32, pia anarudia,

‘Na (a) pa siwenepo, sishuhudiepo ...’. Fumo Liyongo pia anajirejelea katika beti za 40 na kuendelea anaposimulia alivyoiona ‘safina’ ya Mwana Ninga na vile ambavyo alishiriki mapenzi naye.

Kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza umoja, Fumo Liyongo kama mhusika na msimulizi, anasimulia tajiriba zake. Msimulizi huyu anajenga uhusiano wa karibu mno kati yake na msomaji na kufanya aone anachokiona, kusikia anachokisikia na kuhisi anachokihisi. Kutokana na hali hii, msomaji anakuwa katika nafasi nzuri kuelewa tabia, sifa na mtazamo wa msimulizi. Kwa mfano, kutokana na masimulizi haya, tunapata kufahamu kuwa Fumo Liyongo ni mwenye mapenzi tele, ni mwaminifu, mchangamfu. Vilevile, tunapata kujua mtazamo wa mhusika (msimulizi) huyu kuwa mwanamke mrembo ni mrefu na mwembamba.

Hali kadhalika nafsi ya kwanza wingi imetumika katika masimulizi ya *Utendi wa Mwana Ninga*. Nafsi ya kwanza wingi hujumuisha msimulizi pamoja na watu wengine kama wahusika katika kazi ya kifasihi. Nafsi ya kwanza wingi imetumiwa katika ubeti wa 4,5 na 6. Katika beti hizi, mtunzi anawataka watu waje kumsaidia kumsifu mpenzi wake.

Ubeti 4;      Waye wa kiletı,

Wa mbeja wanati,

Tupane sauti,

Tumsifu yanga.

Ubeti 5;      Kisa kuziona,

Baiti kufana,

Yatupe kunena,

Zake Mwana Manga.

Ubeti 6;      Basi tuwakifu,  
                  Yasiwe marefu,  
                  Sifa tusanifu,  
                  Zake Mwana Manga.

Matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yamempa fursa msimulizi kuwahusisha wengine kama wahusika. Vilevile, wahusika hawa wanaweza kuchukuliwa kama hadhira ya msimulizi. Hivyo msimulizi anatumia mbinu hii kuhusisha hadhira yake katika masimulizi. Vilevile, mbinu hii imesaidia kuendeleza maudhui ya ujamaa, umoja, uhusiano bora na ushirikiano katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

Nafsi ya pili pia imetumika katika utendi huu. Katika ubeti wa 1 na 2, msimulizi anarejelea nafsi ya pili anapowaambia watu wapige pembe wawaite watu wengine waje kumsaidia kumsifu mpenzi wake. Wale anaowataka wapige pembe ndio nafsi ya pili. Nafsi ya pili inatumika vilevile katika ubeti wa 15 (...sitaajabuni....) Msimulizi anawataka watu kutostaajabu anayoweza kufanya Mwenyezi Mungu. Sawa na nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili inatumiwa kama njia ya kuhusisha hadhira katika masimulizi.

Hali kadhalika, nafsi ya tatu imetumika katika masimulizi ya *Utendi wa Mwana Ninga*. Nafsi hii imetumiwa kumrejelea Mwana Ninga ambaye pia ni mhusika katika utendi huu. Nafsi ya tatu umoja huonyeshwa kwa matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ‘yeye’ au kiambishi cha nafsi ‘a’. Pamoja na hayo, vivumishi vimilikishi vyenye shina ‘-ake’ hutumiwa kuonyesha umiliki katika nafsi ya tatu umoja. Mtindo huu wa kutumia vimilikishi ndio unatumiwa katika *Utendi wa Mwana Ninga* kuonyesha hali ya Mwana Ninga kumiliki sifa zinazosimuliwa na mtunzi.

Vimilikishi hivi vimetumiwa katika beti nyingi kama vile: yake mitulinga (25), pepo yake (32), ziwavuze / mbavu zake (34), yake safiina (40), yake Mwana Manga (42), nyaoze / nyayo zake (51) na kadhalika.

Matumizi ya nafsi ya tatu inapendelewa sana na watunzi wengi wa tungo za kisimulizi. Nafsi ya tatu humwezesha mtunzi kwa kiwango kikubwa kujitokeza tu kama anayeshuhudia. Hata hivyo, wakati mtunzi mwenyewe anapokuwa vilevile ndiye msimulizi, huwa hawezi kujitenga na matukio katika masimulizi yake. Kwa kutumia mtindo huu, msimulizi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu kusawiri sifa mbalimbali za mpenzi wake. Hivyo, ni mbinu muhimu ya kuwasawiri wahusika, ambacho ni kipengele muhimu cha fani. Pia mbinu hii imemsaidia mtunzi kuwasilisha maudhui ya sifa za mwanamke.

#### 5.4 HITIMISHO

Katika sura hii ya tano, tumehakiki matumizi ya lugha, toni na usimulizi katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumebaini kuwa utendi huu una mbinu za uhuru wa kishairi wa aina mbalimbali, misamiati ya Kingozi, Kiamu na Kiarabu. Vilevile, *Utendi wa Mwana Ninga* una matumizi ya tamathali za usemi kwa wingi. Tamathali za usemi zenye nafasi kuu ni sitiari na tashibibi.

Kwa upande mwingine, tumebainisha kwamba toni ya *Utendi wa Mwana Ninga* inadhihirisha hisia za mapenzi, kuridhika, uaminifu na uchangamfu. Mtunzi ametumia usimulizi katika nafsi ya kwanza umoja na wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu umoja. Vipengele<sup>vya</sup> kifani vya matumizi ya lugha, toni na usimulizi vimehusiana na kukamilishana katika ujenzi wa muundo

usawiri wa mandhari na wahusika na uibukaji wa maudhui. Katika sura ya sita, tunatoa hitimisho la utafiti huu.

## **SURA YA SITA**

### **TATHMINI NA MAPENDEKEZO**

#### **6.0 UTANGULIZI**

Sura hii inahusu hitimisho la utafiti huu. Tunatathmini madhumuni tuliyokuwa nayo mwanzoni mwa utafiti huu. Pia tunatathmini nadharia tete zetu. Hali kadhalika, tunatoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu *Utendi wa Mwana Ninga*.

#### **6.1 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Katika utafiti huu, tulitaka kubainisha vipengele vya fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeweza kuafikia madhumuni haya. Katika sura ya tatu, tumehakiki ploti na muundo wa *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumeona kuwa ploti ya utendi huu ni sahili. Ploti yenye we inatiririka kimfuatano. Hakuna urejelezi nyuma. Msimalizi anaanza kumsifu mpenzi wake kuanzia kichwani mpaka miguuni. Maelezo yake ni ya moja kwa moja. Muundo wake pia umefuata sifa mbalimbali za tenzi kama zinavyoolezwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili.

Katika sura ya nne, tuliangalia vipengele zaidi vya fani ambavyo ni mandhari na wahusika. Tumeona kuwa mandhari yenye we ni ya Uswahilini na pia Uarabuni. Pia tumeona kuwa kuna mandhari ya baharini na msituni. Kuhusu wahusika, tumetambua kuwa wahusika katika *Utendi wa Mwana Ninga* ni wawili ambao ni Fumo Liyongo na Mwana Ninga. Wahusika hawa ni wapenzi. Liyongo pia ndiye msimalizi anayemsifu mpenzi wake.

Pia tumehakiki vipengele zaidi vya kifani katika sura ya tano. Hapa tumehakiki matumizi ya lugha, toni na usimulizi. Chini ya matumizi ya lugha, tumezungumzia kuhusu matumizi ya uhuru wa kishairi na matumizi ya tamathali za usemi. Tumeona kuwa mtunzi wa utendi huu ametumia uhuru mbalimbali wa kishairi kama vile mazida, tabdila, inkisari na uhuru wa kisintaksia. Pia mtunzi ametumia misamiati ya Kingozi na vilevile ya Kiamu na Kiarabu. Mtunzi pia ametumia tamathali za usemi kwa wingi. Tamathali tulizoziangalia ni pamoja na sitiari, tashibihi, chuku, tasifida, usambamba, tashihisi, takriri na nidaa. Sitiari na tashibiha ndizo zinazojitokeza sana.

Vilevile, tumejadili toni katika *Utendi wa Mwana Ninga* na kuona kuwa toni mbalimbali zinajitokeza. Kuna toni ya mapenzi, toni ya uaminifu, toni ya imani, toni ya furaha na kadhalika. Pia tumbaini kuwa utendi huu umechanganya usimulizi wa aina mbalimbali kama vile usimulizi wa nafsi ya kwanza, pili na tatu. Kwa ujumla, madhumuni ya kubainisha fani iliyotumiwa na mtunzi yalitekelezwa katika sura tatu.

Madhumuni ya pili yalikuwa kuhakiki mchango wa vipengele vya fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Tumbaini kuwa vipengele vya fani vina mchango mkubwa sana katika kuwasilisha maana na dhamira ya utendi huu. Tumegundua kuwa dhamira ya mtunzi wa utendi huu ni kumsifu mpenzi wake. Maudhui ya sifa yanabainika kutokana na fani mbalimbali. Hali kadhalika, vipashio vya fani vimesaidia kuleta taswira au picha kamili ya hali ya mambo. Bila ya vipengele hivi vya fani, maana ya utendi huu na taswira zake hazingejitokeza kamili na kwa uwazi. Fani pia imesaidia katika kuupa *Utendi wa Mwana Ninga* uzuri na mvuto wa kuvutia hadhira. Kwa hivyo, fani ina mchango mkubwa sana katika utenzi wa utenzi huu.

Pia tulikusudia kutathmini kufana au kufeli kwa mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* katika utenzi wake. Tumetekeleza madhumuni haya katika sura ya tatu, nne na tano. Kutokana na fani

aliyotumia, tumeona kuwa Fumo Liyongo amefaulu sana katika utunzi wake. Ameweza kuupa *Utendi wa Mwana Ninga* muundo mmoja wenyewe kushikamana vizuri. Vipengele vya fani anavyotumia vimeingiliana vizuri sana. Mtunzi ameweza kuwasilisha dhamira yake ya kumsifu mpenzi wake.

### 6.3 UTATHMINI WA NADHARIA TETE

Nadharia tete yetu ya kwanza ilisema kwamba vipengele vya fani katika *Utendi wa Mwana Ninga* vimeingiliana na kuhusiana katika ujenzi wa umbo au muundo wa utendi wenyewe. Nadharia tete hii tuliweza kuithibitisha kuwa kweli. Tuneona kuwa msuko wa utendi huu umeingiliana sana na usimulizi na uumbaji wa wahusika. Kuelezea msuko wa utendi huu ni sawa na kuelezea usimulizi wake. Vilevile, kuelezea msuko wenyewe ni sawa na kuelezea sifa za mhusika Mwana Ninga. Pia matumizi ya lugha yameingiliana sana na ujenzi wa mandhari, uumbaji wa wahusika, usimulizi na toni. Tamathali mbalimbali zinazotumika zinasaidia kutuelekeza kwa mandhari ya baharini, Uswahilini na Uarabuni katika *Utendi wa Mwana Ninga*.

Nadharia tete ya pili ya utafiti huu ilisema kwamba fani katika *Utendi wa Mwana Ninga* imesaidia kuwasilisha maana katika utendi wenyewe. Tumethibitisha nadharia tete hii kuwa ukweli. Kutokana na matumizi ya lugha, msimulizi ameweza kuwasilisha maana ya sifa katika utendi huu. Tamathali za usemi anazozitumia zinahusiana na sifa za uzuri na urembo. Tumeona akitumia sitiari na tashibihi za vyombo vya mapambo kutoka Uarabuni ambavyo vinadhaniwa kuwa vizuri zaidi. Pia analinganisha na mti wa mnga ambaao ni mrefu na wenyewe miba ili kuleta maana ya mwanamke imara ambaye hawezi kufikiwa kwa urahisi. Msuko wa utendi huu pia unasaidia kutiririsha maana na kuifanya kuwa rahisi kueleweka.

Nadharia tete ya tatu ilisema kwamba mtunzi wa *Utendi wa Mwana Ninga* amefaulu katika utunzi wake. Tumeona kuwa nadharia tete hii ni kweli. Mtunzi amewasilisha sifa za Mwana Ninga kwa uwazi. Ameumba wahusika wake vizuri. Pia ametumia msuko sahili ambao unasaidia kueleweka kwa utendi huu kwa njia rahisi. Fani ya utendi huu imeingiliana vizuri na hatuwezi kutenganisha vipengele vyake mbalimbali. Pia tunapata hisia sawa za mapenzi kama anavyozitoa mtunzi.

#### **6.4 MAPENDEKEZO YA UTAFITI**

Tumehakiki fani katika *Utendi wa Mwana Ninga*. Hata hivyo, baadhi ya vipengele vipana kama vile usimulizi hatujaweza kuvishughulikia kwa undani sana. Tunapendekeza kuwa watafiti wengine washughulikie kipengele hiki cha usimulizi kwa undani. Kwa upande mwingine. Utafiti pia unaweza kufanywa kuhusu maudhui na dhamira ya utendi huu. Fani pia inaweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia tofauti na ya Umuundo. Pia ulinganishi unaweza kufanywa baina ya utendi huu na tenzi zingine za Kiswahili kuhusu fani yake. Aidha, usawiri wa mwanamke waweza kushughulikiwa katika utendi huu.

## MAREJELEO

- Abedi, K. A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es Salaam: East Africa Publishing House.
- Allen, J.W.T (1971) *Tendi*. London: Heinemann Publishers.
- Aristotle (1965) "Poetics" Katika S.T. Dorsch, Aristotle/Horace/Longinus. Harmondsworth:Penguin.
- Culler, J (1975) *Structuralist Poetics: Structuralism, Linguistics & Study of Literature*, Routledge & Kegan Paul Ltd.
- Forster, E.M .(1927) *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.
- Freeman –Grenville,G.S.P (1962) *The East African Coast:Select Documents from the First the Earlier 19<sup>th</sup> Century*:Clarendon Press,Oxford
- Gill, R. (1985) *Mastering English Literature*. London: The Macmillan PressLtd.
- Harries, L.H (1962) *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.
- Harrow, K.W (1991) *Faces of Islam in African Literature*: Heineman Portsmouth H. James Currey; London.
- Hichens ,W. (1972) *Al-Inkishafi*.S.A Nasir. Nairobi: Oxford University Press.

- Holman,C.H. (1960) *A Handbook to Literature*.New York: Odyssey Press inc.
- \_\_\_\_\_, na Harman, W (1986) *A Handbook to Literature*. New York: Macmillan.
- Kezilahabi, E (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heineman.
- \_\_\_\_\_ (1997) “*Creative Writing in Swahili.*” Makala ya Kongamano la Uandishi wa Kibunifu katika Lugha za Kiafrika SOAS, London.
- King'ei, na Amata, J. K (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stante.
- Knappert, J.(1967) *Traditional Swahili poetry. An investigation into the Concepts of E. African Islam as reflected in the Utensi Literature*: Leiden E. J. Brill Publishers.
- \_\_\_\_\_ (1971) *Swahili Islamic Poetry* University of California.Leiden: E. J Brill.
- \_\_\_\_\_ (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*.London: Heinemann Ltd
- Kofa, T (2009) *Uhakiki wa Fani katika Utensi wa Swifa ya Nguvumali Tasnifu ya MA*, Chuo Kikuu cha Nairobi: (haijachapishwa).

- Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- Lambert, H.E (1965) "Some Initiation Songs of the Southern Kenyan Coast." *Swahili 35/1* 49-67
- 
- (mhr) *Ode to Mwana Mnga*: (bulletin No.23 Of the East African Inter-Territorial Language Committee, pg. 56-63)
- Leech, G.N na Short, M.H (1981) *Style and Fiction. A linguistic Introductuion of English. Fictional Prose*. Newyork: Longman Group.
- Mazrui, A na Shariff, I (1976) "A Role on Swahili Poetry." *Katika Jarida la Kiswahili*. Toleo la 46.1 uk 67-70.
- Mbatiah, M. (2001) *Kamus ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Group and Publishing.
- Mnyampala, M (1965) *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Mohammed, S. A (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: E.A.E.P

- Mulokozi, N.M (1975) *Mukwava wa Uhehe*. Nairobi: East African Publishing House.
- Mulokozi, N.M na Sengo T.S.Y (1995) *A History of Kiswahili Poetry*. A.D 1000-2000 University of Dar es Salaam.
- Mulokozi, N. M. (1999) *Tenzi tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI
- Mungai L (2005) *Ulingenisho wa Kifani wa Tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi Mayasa*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).
- Ngara (1985) *Art and Ideology in the African Novel: A Study of the Influence of Marxism on African Writing*. Nairobi: Heineman
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Olali ,T (2004) *The Veneration of The Prophet: The Role of Kasida Hamziyya During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Tasnifu ya PHD (haijachapishwa)
- Osiemo, D.O (1997) *Fani katika ushairi wa mwalimu Hasan Mbega Uhakiki wa upisho wa Malenga na Dafina ya*

## *Umalenga: Tasnifu ya M.A Chou Kikuu cha*

## Nairobi. (haijachapishwa)

## *Practical Criticism. A Study of Literally Judgement:*

London, Routledge.

*Kielezo cha Fasili.* London: Thomas and Nelson.

## *Ushairi: Nadharia na Tahakiki. Dar es Salaam:*

Dar es Salaam University Press.

*Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African

## Educational Publishers.

TUKI (1981)

*Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford.

(2000) *Swahili-English Dictionary*. (2<sup>nd</sup> Edition) Dar-es-

## Salaam: Institute of Kiswahili.

Wamitila. K. W. (2002)

*Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

(2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi:

Focus Publishers.

## (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.*

Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

- Wa Mutiso, K (1985) “*Hurafa ya Uyakinifu katika Hamziyyah*”. Tasnifu ya MA Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).
- \_\_\_\_\_ (1996) “*Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai.*” Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya Shahada ya uzamifu. (haijachapishwa).
- \_\_\_\_\_ (2002) *The Epic of Princess Fatuma.* Mswada. (haujachapishwa).
- \_\_\_\_\_ (2003) *The Epic of the Secrets of all Secrets.* Mswada (haijachapishwa).
- Welleck, R na Warren, A (1949) *Theory of Literature Seminar Study of the Nature and Function of Literature in all its contexts.* Hansworth: Penguin Books Ltd.

## **ODE TO MWANA MNGA**

**H. E. LAMBERT**

Bulletin no. 23 of the East African Inter-Territorial Language Committee.

1. Pijiani mbasi,

Pembe ya jamsi,

Kwa cha mtotosi,

au mwananinga.

5. Kisa kuziona,

Baiti kufana,

Yatupe Kunena,

zake Mwana Manga,

2. Upije na pembe,

Iliao yumbe,

Muwangi uambe,

Kwa ya ndovu kanga.

6. Basi tuwakifu,

Yasiwe marefu,

Sifa tusanifu,

Zake Mwana Manga.

3. Vumi lende mbali,

Lamshe ahali,

Wake na wavuli,

Waye nganga-nganga,

7. Takwanda kitani,

Nduza sikiani,

Hariri laini,

Zake nyele singa.

4. Waye wa kileti,

Wa mbeja wanati,

Tupane sauti,

Tumsifu Yanga.

8. Kitache huramu,

Ni kama rukhamu,

Enga jaizimu,

Taole kuzinga

9. Yake mashikio,  
     Apulikiao,  
     Yatendele tao,  
     Kama kombe nanga.
10. Uso wake mwana,  
     Utengue sana,  
     Napa siyaona,  
     Kwakuta mianga.
11. Nshize zifene,  
     Nta zilingene,  
     Shina lifungene,  
     Kama lalofunga.
12. Ni nyeusi mno,  
     Zaidi ya wino,  
     Zitwalie kono,  
     Ya tandu za mnnga.
13. Mato avikapo,  
     Khasa avuapo,  
     Mtu akiwepo,  
     Hutisha kuyenga.
14. Puaye ajabu,  
     Zivungu hurebu,  
     Ni sita hisabu,  
     Mwenyi kuziwanga.
15. Sitaajabuni,  
     Kuliko Manani,  
     Hata ishirini,  
     Zivungu kupanga.
16. Zake zitefute,  
     Zizidie zote,  
     Ya mkatekate,  
     Mafuta ya kwenga.
17. Miomo nyembamba,  
     Asipoifumba,  
     Atakapokwamba,  
     Helewa mjinga.
18. Kwamba takwambaye,  
     Tatongoa iye,  
     Ajabu menoye,  
     Humwayengayenga.

19. Si ya akhadharu,

Si ya ahamaru,

Hufana na nuru,

Iwaa Manga.

24. Shingoe ni ndefu,

Mwandi sharifu,

Ipambiwe kufu,

Kama za kutunga.

20. Si ya mkakasi,

Si ranji nyeusi,

Ni kufana basi,

Huwa wanda Manga.

25. Ni hidaya njema,

Umbile Karima,

Iyalie nyama,

Yake mitulinga.

21. Kanwa huradidi,

Nyoshi za mkadi,

Au za zabadi,

Ya ngawa na funga.

26. Mafuzi kadiri,

Haya kudhihiri,

Kama bilauri,

Taole kuzinga.

22. Ulimi mpesi,

Wake ni fanusi,

Khasa kidurusi,

Hudighimu yanga.

27. Mikono imie,

Mbinu ziyalie,

Zandaze ni zie,

Za tandu za mnga.

23. Shani ni kieu,

Si kungu mbiavu,

Ni kungu tengevu,

Kungu-kungu Manga.

28. Nyaaze launi,

Kama marijani,

Napa hutamani,

Mwenyi kuziwenga.

29. Makapwae nduza,  
 Mtu kituliza,  
 Mbwene ukimeza,  
 Mte mpakanga.
30. Huteta harufu,  
 Zaidi ya afu,  
 Au matukufu,  
 Mafuta ya Manga,
31. Naapa Wallahi,  
 Asioshabihi,  
 Tanena sahihi,  
 Ya makoma Manga.
32. Napa Siwenepo,  
 Sishuhudiepo,  
 Matunda ya Pepo,  
 Yake Mwana Manga.
33. Yakiwa nguoni,  
 Hutisha uyuni,  
 Yawapo baiyani,  
 Akili hutanga.
34. Ziwavuze mwana,  
 Ziwavu zinana,  
 Hutisha kuvina,  
 Wenyi kumsinga.
35. Maungo yamele,  
 Sarara zilele,  
 Hazitumbalile,  
 Hazi kumpinga.
36. Matumbo makuto,  
 Ndia na masito,  
 Kitovu ni kito,  
 Kuvuta kafunga.
37. Kitovu ni huka,  
 Kezo la kimaka,  
 Mwenyi kumnuka,  
 Pua damu henga.
38. Tawangu ni zito,  
 Kwa nyao za peto,  
 Tena lina kito,  
 Pesi la kuzinga.

39. Wema wa duara,  
 Angalia dira,  
 Usipoidara,  
 Yandapo kuzinga.
40. Yake Safiina,  
 Nalipoiona!  
 Si nyire si pana,  
 Iyalie nyonga.
41. Ngamani kingia,  
 Ili kutungia,  
 Kesa kuzengea,  
 Ngama isikwenga.
42. Ikimekameka,  
 Ikinukanuka,  
 Vumba la kimaka,  
 Yake Mwana Manga.
43. Kwalina mawingu,  
 Na pepo nyengwangu,  
 Zote zombo zangu,  
 Kazifungafunga.
44. Kakundua dumi,  
 Matangaye kumi,  
 Khasa la galime,  
 Shiraa kasonga.
45. Kazungua bao,  
 Kapinga sikio,  
 Mbwene yavutao,  
 Mai henda Manga.
46. Kangia ngamani,  
 Kenda uziwani,  
 Niiepo pwani,  
 Kapiga mzinga.
47. Niinushiepo,  
 Kafanya kitapo,  
 Kasabibu pepo,  
 Kevuza waganga.
48. Ziweoze ndiwa,  
 Ni tako la siwa,  
 Wende hula ngowa,  
 Na kumzimnga.

49. Maondo ni sifa,

Yana maarifa,

Henda kwa misafa,

Na kuiviringa.

50. Tafuze kadiri,

Hazi kudhihiri,

Kowa la zumari,

Taole kuzinga.

51. Nyaoze ashashi,

Vaole ni koshi,

Kazi ya nakishi,

Kwa kazi ya Manga.